

MATARAJIO

 ...kubwa na dogo, kama vile Dk. F. F. Bosworth, mmoja wa wenzangu ambaye hivi majuzi alienda nyumbani utukufuni, karibu umri wa miaka mia moja (Ni wangapi waliopata kumjua Ndugu Bosworth? Nina hakika wengi wenu ninyi watu mlimjua.), alizoea kuniambia, akasema, “Vema, Ndugu Branham, kile tunachotumia kwa uponyaji wa Kiungu, ni kama tu chambo unachoweka kwenye ndoana. Kamwe humwonyeshi samaki ndoana, unamwonyesha chambo, ndipo anapouma chambo, anashikwa na ndoana.” Kwa hiyo hivyo ndivyo tunavyojaribu kuutumia uponyaji wa Kiungu.

2 Ni karama ya Mungu ambayo...na halafu sisi... unawavutia watu, nao wanaona jambo fulani likitukia ambalo wanajua lisingeweza kutukia isipokuwa Mungu alikuwa amelifanya, kwa hiyo inageuza usikivu wao kutoka kwa mambo ya ulimwengu hadi kwa Mungu. Mnaona? Na hiyo ndiyo, sababu ya sisi kusema ni chambo kinachowaongoza wenye dhambi...

3 Kilicho kusudi letu kuu hapa, ni kumnasa asiyeamini apate kumwamini Mungu. Hilo ndilo tunalotaka kufanya, ni kuwa, kumwona mwenye dhambi akiongoka kwa imani iliyo hai katika Bwana wetu Yesu Kristo, na hilo ndilo jambo letu kuu. Jambo la pili ni kujaribu kuwasaidia wagonjwa na wahitaji kupata usaidizi. Na wengi wao, bila shaka, kama ilivyo kote ulimwenguni, hawajiwezi kabisa, isipokuwa Mungu awafanyie jambo fulani, kwa sababu sayansi yetu ya matibabu, baadhi yao wamepita hiyo.

4 Nami niliondoka tu nyumbani jana ambako, ama majuzi, naam, jana, ambako nilimwona Bwana akimchukua mwendawazimu kabisa, ambaye miaka miwili hata hawajui walikuwa wapi, jina lao lilikuwa nani, ama chochote kulihusu, na kuwarejesha katika akili zao timamu, mpaka wahudumu wote wa hospitali hiyo wakasema kamwe hawakuwa wamewahi kuona kitu kama hicho. Mnaona? Mwendawazimu kabisa, msichana mwendawazimu, miaka miwili. Na ninii tu, unapoona kitu kama hicho, tunajua ya kwamba inahitaji Mungu kufanya hivyo, hivyo tu.

5 Unajua ya kwamba mwanadamu hawezi kufanya mambo kama hayo, wala haukupewa mwanadamu, hata hivyo, uponyaji wa Kiungu, kuna aina moja tu ya uponyaji na hiyo ni uponyaji wa Kiungu, hakuna uponyaji mwingine ila uponyaji wa Kiungu. Uponyaji wote hauna budi kuja kupitia kwa Mungu, Zaburi 103:3 ilisema, “Mimi ni Bwana nikuponyaye magonjwa yako yote.”

⁶ Sasa, dawa hutibu, wenye dawa hawadai kutibu, wanadai tu kusaidia maumbile, Mungu Ndiye aponyaye. Nilihojiwa huko kwa Mayo Brothers, na hivyo ndivyo walivyoniambia kule, kasema, “Hatudai kuwaponya watu, tunadai tu kusaidia maumbile huku Mungu akiponya.”

⁷ Kwa maneno mengine, kama una jeraha mkononi mwako, vema, watalishona, hawaliponyi. Kama una kidole tumbo kibaya, wanaweza kutoa hicho kidole tumbo, lakini hivyo tu ndivyo wanavyoweza kufanya. Kama umevunjika mkono, unaweza kuurudisha mkono. Ni nani atakayetoa kalisi na kile kinachohitajika ili kuunganisha mfupa huo? Inahitaji, kujenga upya seli kunahitaji uhai, na *uhai* ndio unaosababisha uponyaji. Tunaweza kukata, kufanya upasuaji, na kadhalika, bali hatuwezi kuponya, Mungu hana budi kufanya hivyo Mwenyewe, huo ni uzidishaji wa seli. Huo huja tu kupitia kwa Mungu, huyo Ndiye tu anayeweza kufanya jambo hilo.

⁸ Tunaweza kumfanya mtu wa kimitambo, ambapo angeweza kuinyosha mikono yake, na karibu awazie, bali hatuwezi kujenga seli. Hiyo ni kusema, Mungu pekee hufanya hivyo. Kwa hiyo, Yeye ni Bwana, huponya magonjwa yetu yote. Tunaweza kung’oa jino, lakini ni Nani atakayeikomesha damu? Na ni Nani atakayeponya mahali lilipotoka? Mungu asipopaponya, kamwe hatutaponywa. Hiyo ni kweli.

⁹ Vipi kama nilikuwa hapa nje nikizungusha mpini wa gari langu, bila shaka hiyo ni muda mrefu uliopita, nadhani, katika siku za kale za Muundo T wa kibyongo, sasa, wakati walipokuwa wakiwasha gari la kale kwa kuzungusha mpini, vipi kama ningevunja mkono wangu, ningeingia ndani mbio, niseme, “Tabibu, uponye mkono wangu upesi sana, ni—ninapaswa kumaliza kuzungusha mpini wa gari langu?”

¹⁰ Vema, angesema, “Unahitaji uponyaji wa akili.” Vema, hiyo ingekuwa ni kweli. Mnaona? Angesema, “Vema, mimi, angalau ninaweza kurudisha mkono wako, lakini *Kitu fulani* kilicho juu kuniliko hakina budi kuuponya.” Hiyo ni kweli. Anaweza kuurudisha, na huo ndio wajibu wake, hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya, kwenda na kumwacha aurudishe, lakini aponyaye ni Mungu. Kwa hiyo, siamini ya kwamba kuna kitu kama mponyaji wa Kiungu nje ya Mungu, ninaamini ya kwamba Mungu ndiye Mponyaji pekee aliyepo.

¹¹ Kwa hiyo mara nyingi watu wamesema, “Ndugu Branham, yule mponyaji wa Kiungu.” La, mimi si mponyaji wa Kiungu zaidi ya vile mchungaji alivyo mwokozi wa Kiungu. Kwa hiyo mimi, tunahubiri tu Injili. Injili ya Bwana Yesu Kristo ni habari njema kwamba Kristo alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi *tuliponywa*. Ni jambo ambalo limepita. Mnaona? Kristo alitufanyia yote yaliyopaswa

kufanywa, na yote yanayoweza kufanywa, tayari yamefanywa. Ninaamini ya kwamba jambo pekee tunalopaswa kufanya ni kukubali yale Yeye aliofanya, yale ambayo tayari yamefanywa.

¹² Na sasa, mhudumu, mhudumu yeyote, ana haki sawa tu ya kuwaombea wagonjwa, ama walei, kama tu mtu mwingine yeyote, kwa sababu Yeye alisema, “Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate...mpate kuponywa. Kwa maana kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidii.” Ninaamini ya kwamba kuna nguvu katika maombi. Nimeona majibu ya moja kwa moja kwa maombi, lakini sijawahi kumponya mtu yeyote maishani mwangu, lakini nimemwona Mungu akifanya mengi sana. Kwa hiyo ni—ninaamini ya kwamba ni imani ya mtu binafsi katika kazi ambayo tayari imekamilika.

¹³ Sasa, unasema...Ningesema hapa usiku wa leo, “Ni Wakristo wangapi?” Mikono *mingi sana* ingeinuliwa. “Ni wangapi waliookoka mwaka uliopita?” Mikono *mingi sana* ingeinuliwa. “Ni wangapi waliookoka, labda, juma moja lililopita?” Labda kungekuwa na mikono miwili au mitatu itakayoinuliwa. Natofautiana, hu—hukuokoka mwaka mmoja uliopita, ama hukuokoka siku mbili ama tatu zilizopita, uliokolewa miaka elfu moja mia tisa iliyopita pale Kalvari, bali uliukubali mwaka uliopita, ama uliukubali juma lililopita, mnaona, ama siku mbili zilizopita. Na jambo lile lile, “kwa kupigwa Kwake wewe *uliponywa*,” unaona, “*uliponywa*,” wakati uliopita, “uliponywa.” Sasa, unaweza kuukubali usiku wa leo, ama unaweza kuukubali kesho usiku, ama wakati wowote unapoukubali, mbona, ni wako, kwa hiyo ni juu yako wakati unapotaka kuukubali juu ya misingi hiyo.

¹⁴ Naye sasa ni Kuhani Mkuu, Waebrania 3, ameketi mkono wa kuume wa Mungu Mwenyezi Mbinguni, akituombea tunapokiri. Sasa, neno lililotumiwa pale katika—katika Kitabu cha Waebrania linatumiwa, katika Toleo la King James, linatumiwa *kukiri*, lakini *kukiri* na *kuungama* ni kitu kile kile. Unakiri jambo fulani ama kuliungama, unakiri ya kwamba unaamini ya kwamba Yeye ana...Alijeruhiwa kwa makosa yako kwa kupigwa Kwake wewe uliponywa. Kwa hiyo Yeye ni Kuhani Mkuu kutuombea tunapokiri, wala hawezi kutufanyia lolote, mpaka kwanza tulikubali na kuungama.

¹⁵ Sasa, tungeweza kushuka madhabahuni na kuomba mpaka tukawa, mpaka tukalala kifudifudi tukafa, mpaka tuamini, na kuikubali neema Yake ya msamaha, tungali tumepotea. Haidhuru tungeweza kupiga mayowe kwa sauti kubwa jinsi gani, ama tungeweza kukaa muda gani, ama tungeweza kukaa bila chakula muda gani, mpaka moyoni mwetu Mungu atupe ufunuo kwamba Yesu Kristo alikufa apate kutuokoa, nasi tuukubali kama mali yetu binafsi, ni jambo ambalo Kristo alinifanyia, alikufanyia, na kwa yeyote atakayeliadini, basi

umeokoka kwa sababu umeamini hilo, na unaponywa vivyo hivyo.

Mara nyingi, watu husema, “Na—napenda kuhisi kama nimeponywa.”

¹⁶ Yesu kamwe hakusema, “Uliuhisi?” Alisema, “Uliamini?” Jambo ndilo hilo. “Unaliamini?” Hisia hazina uhusiano wowote nalo, ni imani yako. Kama ningefanya jinsi nilivyojisikia, ningekuwa katika hali mbaya mara nyingi. Hiyo ni kweli, ndugu? Nadhani sote tungefanya hivyo. Lakini si jinsi ninavyojisikia, ni yale ninayoamini kwamba Yeye amefanya. Si hisia zangu, ni imani yangu katika nini? Kazi iliyomalizika pale Kalvari.

¹⁷ Sasa, katika hili labda kuna wengi . . . Hii ndiyo mara yangu ya kwanza kuwa katika mji wenu, ninaamini ni mara yangu ya kwanza huku Virginia, kuwahi kuwa na ibada Virginia; kuzunguka ulimwengu mara saba, na hata hivyo sijawahi kuwa Virginia. Hilo si ni baya sana? Vema, daima wanasema, “Unaweka akiba kilicho bora zaidi, mwishoni.” Je, hivyo ndivyo ilivyo, ndugu? “Yaliyo bora zaidi huja mwisho.” Kwa hiyo, tunatumaini ya kwamba hilo ni kweli kabisa.

¹⁸ Laiti watu wote, kama wale ambao tumekutana nao tangu tumekuwa hapa! Hakika tumekutana na watu wazuri sana. Na labda nimekuwa nikikutana na watu wa—wananchi tu, labda hata si Wakristo. Na basi Wakristo watakuwaje, endapo raia wako hivyo, wasio Wakristo? Watakuwa wazuri sana. Kwa hiyo sasa, mkutano unaweza tu kuwa chochote watu watakachoufanya.

¹⁹ Sasa, Mungu yuko tayari kama tuko tayari, bali tuna sehemu yetu ya kutekeleza, kila mtu binafsi ana sehemu yetu ya kutekeleza, siwezi tena hata kidogo kufanya uamsho kutoka kwake, wala mkutano. Wala hakuna mtu mmoja binafsi, ama hakuna wawili au watatu wenu tu, itahitaji sisi sote pamoja, tukifanya kazi pamoja, kupitia kwa Bwana Yesu Kristo, kuona jambo fulani likitimizwa hapa katika mji huu, wakati tumekusanyika pamoja kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Na, ndugu, dada, tunaishi karibu na mwisho, sote tunajua hilo. Ha—hakuna . . . pamoja na . . .

²⁰ Kama ungekuwa umesafiri pamoja nami katika mwaka uliopita, ama kitu kama hicho, unge—ungejua hiyo ni kweli, unaona, kwamba tuko—tuko katika hali ya kutetemeka, na wakati wa mwisho umekaribia. Na mambo haya, tunapoendelea mbele katika hili juma, tutakuwa tukiyawasilisha, yaliyotukia, na yale yanayokaribia kutukia, na kama mnavyoona kwenye magazeti yenu, matangazo ya televisheni, na kadhalika, halafu mtasikiliza kutoka kwenye Maandiko, na yale Roho Mtakatifu asemayo.

²¹ Sasa, nadhani, ninaamini kwa kawaida sisi hufunga karibu saa saba, sivyo, ama kitu kama hicho? Saa saba au nane

asubuhi? Inatupa kama wakati wa kuninii, jamaa wa Full Gospel kuhudhuria ibada yao. Wakati mwingine, hio—hiyo, mnaona, sasa, msiondoke, nilikuwa nikitania, nilikuwa tu nikitania kuhusu hilo. Kwa kawaida, tunaachilia yapata saa tatu, ama saa tatu na nusu, na halafu, pamoja na mstari wa maombi. Kwa hiyo, nafikiri ya kwamba pamoja na kusa- . . . walinzi, nadhani, watatuambia ni kiasi gani, ama ni muda gani tunaweza kuuweka ukumbi wazi, ama chochote kile.

²² Sasa, lazima mwingie kwenye simu, lazima mwanze kuwapigia watu simu, na—na hebu. . . Nawaambieni sasa, nitawaambia jinsi ambavyo sisi, ninaamini, tunavyouendeleza mkutano, ama, pamoja na hawa ndugu. Basi—basi kumbukeni, wakati wowote unapojisikia ya kwamba unataka mtu fulani kuombewa, yeyote wa hawa ndugu hapa, wanaamini Injili ile ile ninayohubiri hapa, mnaona, naye mchungaji wenu ana haki ya kuwaombea kama mtu yeyote mwingine. Hapa tunakuja pamoja, ninaamini imeandikwa katika Maandiko, Bwana alisema, “Ikiwa watu wanaoitwa kwa Jina Langu watakusanyika pamoja, waombe, basi nitasikia kutoka Mbinguni, niiponye nchi yao.”

²³ Kwa hiyo tunaamini ya kwamba maombi ndiyo silaha yenye nguvu kuliko zote iliyowahi kuwekwa katika ulinzi wa mwanadamu. Mnajua, maombi wakati mmoja yalibadilisha nia ya Mungu. Mlijua hilo? Hakika yalibadilisha. Sasa, Hezekia aliambiwa na nabii Isaya, ya kwamba atakufia kwenye kitanda kile, ndipo Hezekia akaelekeza uso wake ukutani na kulia kwa uchungu, na kumwomba Bwana a—apate miaka kumi na mitano zaidi ya maisha.

²⁴ Ndipo Mungu akamtuma tena nabii huyo moja kwa moja, kasema, “Nimemsikia.” Naye akaachiliwa kwa wakati huo, mnaona, wakati Mungu alikuwa tayari ametangaza kifo chake. Lakini Yeye alimwachilia, kwa sababu aliomba. Kwa hiyo kama maombi yana nguvu *hivyo*, yanaweza kufanya nini? Jamani, hatutambui jinsi yalivyo makuu.

²⁵ Sasa, kote katika mkutano, wakati kila usiku tukijaribu kuweka msingi, basi mtu anapoingia, labda baadaye kidogo, labda kesho usiku, halafu labda kesho yake, wageni fulani wakiingia, huenda wakaona jambo fulani likitukia hata wangesema, “Vema, kamwe sielewi,” basi wasipoelewa, basi unachukua Maandiko na kuwaonyesha Kwake.

²⁶ Sasa, kama ukiwahi kuona tendo lolote hapa jukwaani, ama chochote ninachozungumzia hapa jukwaani ambacho si cha Maandiko kabisa, basi unawajibika kwangu, kama Mkristo, kuuvutia usikivu wangu kwake. Kwa sababu kweli ninaamini kwamba Mungu hufanya mambo ambayo hayajaandikwa katika Neno, ninaamini angeweza. Angeweza kufanya lolote alilotaka kufanya, Yeye ni Mungu. Lakini almuradi Yeye anafanya yale

aliyoahidi kufanya hilo litatosha kwangu, a—atimize tu ahadi Yake, na—napenda hilo. Nami ninaamini ya kwamba Neno la Mungu ndilo Msingi, ninaamini ni Neno la Mungu. Na ni msimamo wangu, maisha yangu, na imani yangu yote imewekwa msingi juu ya Neno.

²⁷ Basi hivi ndivyo ninavyowataka mliamini sasa: Kwamba Mungu ha—hana kikomo, Yeye yuko kila mahali, anajua yote, Naye ni Mwenyezi Mungu, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, hawezi kubadilika na awe Mungu. Na chochote Mungu afanyacho wakati mmoja, anapofanya uamuzi Wake, uamuzi huo hauna budi kudumu milele, hauwezi kubadilishwa kamwe. Mungu, kama Mungu akifanya uamuzi mwaka huu, kisha mwaka ujao aubadilishe, hiyo inaonyesha ya kwamba Yeye hakuwa Mungu, maana Yeye hana kikomo, nasi tuna kikomo.

²⁸ Sasa, tunaweza kufanya uamuzi, ninaweza kufanya mmoja usiku wa leo, katika dakika kumi itanibidi kuubadilisha, kwa sababu mimi—mimi hukosea mara nyingi, nyingi sana, wewe hukosea, pia, bali si Mungu. Kwa hiyo kama akiwahi kufanya uamuzi, basi huo hauna budi kuwa ndio uamuzi Wake milele.

²⁹ Namna hii: Kama mtu akipata kuja kwa Mungu naye alijua amepotea na alitaka kuokoka, naye Mungu akamwuliza, na kuweka msingi juu ya *kama angeli*amini, Naye akamwokoa mtu huyo, mtu anayefuata anayetaka wokovu, Yeye hana budi kumfanyia mtu *huyu* vile vile alivyofanya wakati huo. Hana budi kutenda vile vile *hapa* kama alivyotenda *pale*, la sivyo alikosea mara ya kwanza. Mnaona? Hana budi kubaki Mungu. Ninii Yake. . . Na iwapo *Hili* si Neno Lake, basi Yeye si Mungu, mnaona, kwa sababu, *Hili* ndilo alilosema, na kama halitimizi Neno Lake, basi hawezi kuwa na Neno Lake.

³⁰ Hakuna mtu aliye na thamani zaidi kuliko neno lake. Kama—kama kupeana kwangu mkono, na ahadi yangu kwa ndugu zangu haitoshi, kwamba inanibidi kutia sahihi makaratasi mengi, na mengi ya *haya*, *yale* hu—huko ni kutokuaminiana. Ni—ninaninii tu, inakubidi kuamini ninayokwambia, nami sina budi kuamini yale unayoniambia. Na kama—na kama hatuwezi kuaminiana, basi kama neno langu halifai kitu, basi mimi sifai kitu.

³¹ Na iwapo Neno la Mungu halifai kitu, basi Yeye si mzuri, Yeye si bora kuliko Neno Lake. Nami nitasema hivi, ya kwamba Mungu hutimiza kila Neno alilosema na kila ahadi aliyosema. Na kama utachukua msimamo mzuri wa kiakili juu ya ahadi yoyote ya Kiungu Mungu aliyowahi kutoa, Yeye ataitimiza. Kama unaweza tu kuchukua msimamo mzuri, na—na kuamini kwa moyo wako wote. Unaona?

³² Mtu binafsi, si kwamba inakubidi kuwekewa mkono na mtu kwa mhemuko fulani. Loo, jamani, kuna mihemuko mingi sana siku hizi, isingeweza kuwa ni ya kweli. Lakini Neno la Mungu lingali ni kweli. Unaona? Ni la kweli. Misisimko niliyo nayo, sijui

lolote kuihusu, bali ninajua ya kwamba Neno la Mungu ni kweli. Kwa hiyo, basi wakati Mungu anaposema jambo lolote, halina budi kubaki hivyo daima, na hivyo ndivyo ninavyoliamini. Nimeyachunguza, na historia, na yale aliyosema, na, yangetukia na kote katika nyakati, na Nyakati za Kanisa, na kadhalika, na kuliona likiafikiana, mpaka nimeridhika kwamba Yeye ni Mungu, na kila Neno ni kweli, Naye hutimiza Neno Lake pamoja na watu Wake.

³³ Sasa, jinsi tunavyofanya jioni moja, yapata saa moja kabla ya ibada kuanza, kusudi isikatize utangulizi, tunawatuma hao wavulana na kumpa mtu binafsi kadi za maombi. Na kila jioni tunafanya hivyo, kwa sababu kwanza, hivi ndivyo tulivyofanya: Tulipoanza kwa mara ya kwanza... Vema, sasa, bila shaka ikiwa tu ni kama huu hapa, mbona, hata isingetulazimu kusambaza kadi ya maombi tukiwa na kundi dogo kama hili, mnaona. Lakini tunapokuwa na makundi makubwa... ambapo tunatarajia kupajaza mahali hapa kabisa usiku wa leo, au kitu kama hicho.

³⁴ Sasa, ndio kwanza tuondoke Vandalia, Visalia, ilikuwa, Illin... , ama, California, na usiku wa kwanza lile ghala kubwa la silaha kule, walirudisha mamia na mamia, kisha usiku wa pili wakaongezeka maradufu zaidi na zaidi. Tukaenda kwenye uwanja wa maonyesho, na kuna watu wa kutosha kule, saa tisa iliwabidi kufunga malango, kabla hata hamjaingia katika sehemu hizo, mnaona.

³⁵ Ninii tu, wakati mkutano unapoanza, na watu wanaanza kuninii, wenye mioyo yenye njaa wanaanza kuona kwamba... Vema, ni—ni Roho Mtakatifu akitenda kazi miongoni mwa watu. Mnaona? Si mhubiri fulani aliye na imani ya hali ya juu, ya ajabu-ajabu, siamini katika mambo hayo. Ninaamini ya kwamba imani huja kwa kusikia Neno la Mungu, naye mtu binafsi anapaswa kuyanyosha maisha yake na kujiweka sawa na Mungu, iwapo anatarajia kuponywa. Hiyo... Ni—ninaamini ya kwamba uponyaji unadumu, ni kwamba huyo mtu binafsi hana budi kujifanya sawa na Mungu.

³⁶ Huku kote kuwawekea mikono wenye dhambi, na kuwaambia, “Hilo ni sawa, sahau tu hilo, Mungu atakuponya kwa vyovyote vile,” sasa, siamini hilo, ninaamini mtu anapaswa kujisafisha, na kuwa sawa na Mungu, na kujirekebisha, na kuja, na kumwishia Mungu, na kufanya yaliyo mema, na huo ndio uponyaji wa kudumu. Miaka hii thelathini na mmoja nimeona hiyo ni kweli, kwamba mwanamume au mwanamke aliye tayari kujipatanisha na Mungu, Mungu atajipatanisha nao. Mnaona? Inakubidi kujipatanisha na Mungu.

³⁷ Kwa hiyo basi sababu ya sisi kufanya jambo hili, wakati tulipoanza kwa mara ya kwanza, tulikuwa tukiwatumia wachungaji, kila mchungaji aliyekuwa akishirikiana, kadi mia

moja, vema, kwa ajili ya kusanyiko lake na kwa wagonjwa ambao angekuwa akiwaalika, na kadhalika. Vema basi, kuhusu yule mchungaji wa kwanza, wengi wao wamekuwa kwenye mikutano hapo kabla, bila shaka, nadhani, vema, yapata mchungaji wa kwanza aliyelipandisha kundi lake, hilo lilitosha, kwa hiyo tusingeweza kufanya hivyo.

³⁸ Kwa hiyo basi tukawazia, vema, tungegawa tu kadi za maombi siku ya kwanza tulipokuwa kule, na kumpa kila mtu kadi za maombi. Halafu basi, bila shaka, hilo lilitosha, mtu yeyote aliyekuja, vinginevyo mbali na siku ya kwanza, mbona, basi hawakupata nafasi, kuingia kwenye mstari wa maombi, maana tulikuwa na za kutosha kule kudumu.

³⁹ Kwa hiyo basi tukaanza kugawa kadi za maombi kila siku. Halafu basi, wakati tungewasimamisha, labda, kumi na watano ama ishirini, wowote tuliwapata usiku huo, vema basi, wale tu tungeweza kuwaleta humo jukwaani, bali tukawaona hao watu, kama hawatakata namba fulani, ama kadi moja hadi kumi na tano ama ishirini, wangeitupa tu sakafuni, hawakuitaka, wasingelitwa.

⁴⁰ Kwa hiyo basi nikawazia, vema, nitamchukua mtoto mdogo hapa mbele nimwache aje hapa na kuhesabu, mvulana mdogo, kama maskini mvulana huyu anayeniangalia hapa amevaa tai nyekundu, koti la michezo, nami, yapata ukubwa wa mtoto wangu Joseph *pale*, nami ni—ningemleta mmoja wa hao jamaa wadogo aje huku, nami ningesema, “Unaweza kuhesabu, Mwanangu, au Dada?”

“Naam.”

⁴¹ “Hesabu.” Naye angeanza kuhesabu, ama binti, na popote waliposimamia, ningeanzia papo hapo. Amini usiamini, mama alijua mahali hasa pa kumwambia Junior asimamie penye kadi yake, kwa hiyo tungali tuna wanadamu, mwajua, tunahusika nao.

⁴² Na kwa hiyo basi—basi nikamchukua mhudumu mmoja agawe kadi, ndipo basi, katika dhehebu lake, kama hakuonyesha upendeleo kidogo tu, ilisababisha hisia fulani kwa hao ndugu.

⁴³ Ndipo nikamchukua ndugu yangu agawe kadi za maombi, ama, kabla ya hapo nilimchukua mtu mwingine, nikamchukua tu mtu wa nje, nami nikamkamata akiuza kadi za maombi, kwa hiyo basi ilinibidi kumwondoa huyo.

⁴⁴ Kwa hiyo nikamchukua ndugu yangu, naye...Na kwa hiyo, sasa ninaye mwanangu, halafu wavulana wawili, mmoja wao ni mmoja wa wenzangu, Ndugu Gene Goad, nadhani ametambulishwa, na Ndugu Leo Mercier, yuko hapa mahali fulani, na mwanangu, Billy Paul, wako hapa mahali fulani, mmoja wao atakuwa akigawa kadi za maombi. Kwa kawaida Billy hufanya hivyo mwenyewe, kwa sababu Leo na Gene, Gene

husimama kwenye vinasasauti, na—na Ndugu Leo, nafikiri, yuko kwenye vitabu.

⁴⁵ Sasa, ndipo basi tunazigawa hizo, na sasa hivi ndivyo tunavyofanya, kusudi kila mtu ajue, tunashuka hapa na kuchukua kadi, na kushuka mbele za watu, na kuzichanganya zote, papa hapa jukwaani, ili mwone kadi zinachanganywa. Kwa hiyo nanii, yeyote yule anayezigawa, hajui ni nani amemp-... ni nani anayepata namba ipi. Mmoja wenu anakuja hapa, na kusema, “Nina namba moja, hiyo inamaanisha *ndiyo*. Naam, bwana.” Wa pili, aseme, “Mimi ni namba mbili, hapa.” Vema, bila shaka, huenda *huyu* huenda akapata moja, anayefuatia, huenda akapata arobaini na tano, sitini na mbili, na kadhalika, hujui itakuwa wapi.

⁴⁶ Vema, basi, unaona, unasema, “Vema, mimi... Vema, kama sikupata namba moja hadi kumi na tano, afadhali niende nyumbani.” La, la hilo silo. Unaona? Hakuna ajuaye basi wakati nitakaposhuka, popote Roho Mtakatifu anaponiongoza kuanzia, labda kuanzia moja hadi ishirini, ama kuanzia ishirini hadi sitini, ama kuanzia tisini kurudi hadi thelathini, ama mahali fulani namna hiyo.

⁴⁷ Kwa hiyo basi, ni ninii tu, tunajisikia tu, kwa njia hiyo, ni vile Roho Mtakatifu alivyo na njia ya kulitenda, mnaona, kuwaingiza ndani. Nafikiri hivyo ndivyo hasa, hivi ninyi ndugu hamfikiri hivyo ndiyo? Nimekuwa nikifanya hivyo sasa kwa miaka, loo, minne au mitano, au sita iliyopita, kitu kama hicho. Na kwa hiyo, baadaye, utakapopata kadi yako ya maombi hata hivyo, ishikilie, kwa sababu usipoitwa usiku wa kwanza, hatimaye tutaifikia mwishoni.

⁴⁸ Sasa, halafu hizo kadi za maombi tunaziita *kadha* kila usiku. Ikiwa mimi... Bwana akiniongoza kufanya vile... Ndio kwanza tupate mafanikio makubwa sana niliyowahi kupata Marekani kwa kufanya namna hii, hivi majuzi tu.

⁴⁹ Na sasa, ibada yenu kuu huanza saa ngapi, yapata saa moja u nusu? Saa moja na nusu. Afadhali muwe hapa kati ya saa kumi na mbili u nusu na saa moja basi, Nakisia, ama kitu kama hicho, ama, saa kumi na mbili u nusu hadi saa moja na nusu. Msichelewe zaidi ya... Afadhali mje mapema mwezavyo, maana mara kadi *kadhaa* zikigawiwa, mbona ni—ni hizo tu. Basi waleteni, waleteni wapendwa wenu, marafiki wenu walio wagonjwa na muwalete, wapigieni simu, kesho, shukeni mje mpate kadi ya maombi kesho—kesho jioni, kati ya saa kumi na mbili u nusu na saa moja na nusu kwenye lile jumba kuu la mikutano.

Hamna ibada za alasiri popote, nadhani, ndugu? Vema.

⁵⁰ Wakati mwingine wanazigawa namna hiyo katika ibada ya alasiri, haiwalazimu kujipumbaza nazo usiku, lakini kama sisi... katika kanisa fulani, ama mahali fulani, lakini kama

wakifanya hivyo, itakuwa sawa. Shukeni tu mje kesho alasiri, kati ya saa kumi na mbili u nusu na saa moja u nusu.

⁵¹ Halafu basi, tunatarajia kuwa na ibada kila usiku. Nitazungumza kila usiku, Bwana akipenda. Yule meneja, hakuna mtu hapa juu, ila mimi na hao wavulana tu. Na kwa hiyo, tunaninii. . . Nasi tutajaribu, basi, kila usiku kuwaombea wagonjwa, kuwaita wenye dhambi madhabahuni, kufanya kazi pamoja na ndugu zetu, tufanye yote tuwezayo, tufanye huu uwe ndio mwanzo wa uamsho, uamsho wa mtindo wa kale ambao utaitikisa Virginia nzima, kwa namna ambayo kamwe haijatikiswa hapo awali, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Kila kanisa lijae na kusongamana, huku watumishi wa Mungu wakiihubiri Injili kuliko walivyofanya hapo awali, na wenye dhambi wakija Kalvari, na wagonjwa wakiponywa katika kila kanisa, na utukufu wa Mungu ukienda kila mahali, hiyo ndiyo shauku ya mioyo yetu.

Sasa, nina furaha nina saa hii ndogo *hapa*, nami natumaini ni karibu tu, *ni* sahihi, sahihi kabisa, kulingana na saa yangu.

Kwa hiyo sasa, ninataka tu kusoma Andiko, na kufanya mazungumzo kidogo kwa ajili yenu, usiku wa leo.

⁵² Na sasa kumbukeni, tuko hapa si kwa ajili ya kitu kingine. . . Hatuko hapa kuwakilisha dhehebu lolote, kwa sababu mimi—mimi si mfuasi wa kanisa lolote la kimadhehebu. Niliwekwa wakfu kuwa mhudumu wa Baptisti ya Kimishenari, nami nikahudumia maskani huko Jeffersonville kwa muda wa miaka kumi na saba, kisha nikaenda kwenye huduma ya umishenari yapata miaka kumi na mitano iliyopita, na nimekuwa hudumani tangu wakati huo.

⁵³ Basi nilipotoka nje kuwaombea wagonjwa, niliacha tu kanisa, ama kuliacha hilo dhehebu, kwa sababu hapa nje—ninapata kila kitu, vyote pamoja. Halafu ni—ninahisi ya kwamba hivyo ndivyo Bwana alivyo na watoto Wake, kila mahali. Kila mwanamume aliyezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu ni ndugu yangu, na kila mwanamke ni dada yangu, aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu.

⁵⁴ Kwa hiyo siwakilishi shirika lolote. Kama nilikuwa hapa mjini, kwa waongofu, ningejiunga na moja ya makanisa haya mazuri hapa yanayoamini jambo lile lile ninaloamini, kwa hiyo hivyo ndivyo ni—ningelifanya mimi mwenyewe; unajichagulia mwenyewe kufanya lolote utakalo.

⁵⁵ Halafu basi hatuko hapa kwa ajili ya pesa, ninawatakeni mjue hilo, hatuko hapa kwa ajili ya pesa, la, bwana. Nina umri wa miaka hamsini na mmoja, nimekuwa mhudumu kwa miaka thelathini na mmoja, nami nimehubiri miaka kumi na saba kwenye ninii, maskani ya Kibaptisti huko Jeffersonville, Indiana, kamwe sikuchukua sadaka maishani mwangu mwote. Nilihubiri miaka kumi na saba bila hata peni moja ya chochote,

yeyote wa wadhamini angeweza kuwaambia hilo, sikuchukua hata peni moja, nilifanya kazi kwa ajili ya riziki yangu.

⁵⁶ Hata nisingefanya hivyo sasa, kama ningeweza kulipia mkutano hii. Jambo pekee ninalofanya ni kuja hapa na kufanya gharama ya hili jengo, na gharama zozote zinazoambatana na huu mkutano ndizo tu ninazohusika nazo. Lipieni tu kitu hicho na hilo—hilo latosha, siwadaai chochote.

⁵⁷ Tuna vitabu, lakini vitabu hivyo, ninanunua vitabu hivyo kwa kupunguziwa asilimia arobaini, si—si kwa sababu ni kitu cha kutafuta pesa kwa sababu nitapata hasara kwake, bali kuwapelekea watu Ujumbe. Hizo kanda zinatoka kwenye Misheni ya Sauti, kundi lingine ambalo haliko pamoja nasi. Ni, vema, wanatengeneza hizo kanda kwa ajili ya maskani, ambapo wako katika mapatano ya namna fulani pale kwamba wanatengeneza hizo kanda, lakini kwangu mimi, la.

⁵⁸ Wakati mwingine mwishoni mwa mkutano, kama madeni yote yamelipwa, wananipa sadaka ya upendo. Kama hawajamaliza kulipa madeni, hawanipi chochote. Na kama wakinipa sadaka ya upendo, ninairudisha ku—ku—kulipa madeni. Tunataka kuondoka katika mji huu pasipo kudaiwa hata peni moja, kama ikitulazimu kutuma mtu nyumbani, tupate pesa mahali fulani, tutafanya hivyo, mnaona, bali hatuachi madeni yoyote, kamwe hatujayaacha bado.

⁵⁹ Tunataka kudumisha jina letu safi, na wazi, na bila lawama, kwa sababu tunakutana na wagonjwa, tunakutana na Shetani mahali pake, nasi tu—tunataka tuwe ma mikonu safi, kusudi tunapokuja kuwaombea wagonjwa, tupate kuwa waaminifu, na wenye haki, na bila hila yoyote. Tunasimama papa hapa mbele za Mungu kama watumishi Wake, nasi tunataka kuwa waadilifu, na safi, na wazi kwa kila mtu. Nami nawatakeni mjue basi ya kwamba hakuna mvuto wa pesa wala hakuna kitu kuhusu hilo, ha—hatuko hapa kwa ajili ya hilo. Nasi tunawapenda tu, na tumekuja kushirikiana nanyi.

Na kama Ndugu Bosworth alivyoniambia siku moja, akasema, “Ndugu Branham, unajua *ushirika* ni nini?”

Nikasema, “Nafikiri hivyo, Daktari.” Nikasema, “Nafikiri mimi. . .”

“Vema,” kasema, “hivi ndivyo ulivyo: Ni *jamaa* wawili katika *meli* moja.”

⁶⁰ Nami nikasema, “Hilo ni kama tu...?...jamaa wawili katika meli moja.” Kwa hiyo tunatamani hilo, laiti tungaliweza kuingia kwenye maskini mashua yenu, nanyi mngeweza kuingia kwenye mashua yetu tunaweza kufanya ushirika sisi kwa sisi, wakati tukivua samaki humu mjini kusudi tumvute kila mtu aliyepotea tuwezaye kumwingiza katika Ufalme wa Mungu.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa, kabla hatujazungumza na Mwandishi, kabla hatujasoma Neno Lake.

⁶¹ Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe, usiku wa leo, kwa majaliwa haya ya kusimama kwa mara yetu ya kwanza katika jimbo hili kuu la Virginia, jinsi ambavyo miaka mingi iliyopita babu zetu walitua hapa, jimbo hili kuu limekuwa na maana kubwa kwa Muungano wetu. Bwana, ninaomba kwamba, kwa namna fulani, ya kwamba katika jimbo hili kuu sasa, kwamba Wewe utaanzisha uamsho ambao utaninii, utajulikana kote ulimwenguni.

⁶² Jalia itokee hoja kwa Mungu, Roho anayewaka moto wa Roho Mtakatifu ambaye atawaokoa waliopotea, na kuwaponya wagonjwa, jalia vipofu waone, viwete watembee, viziwi wasikie, mabubu kuzungumza, wenye dhambi waokoke katika Ufalme wa Mungu, kila kanisa limeangaziwa tu na Uwepo Wako, mpaka kote ulimwenguni watasikia kutoka kwenye mkutano huu mkuu. Sasa, tunaweza kuomba hilo, Bwana, na kuliadini, sasa tusaidie kulishughulikia kusudi hilo. Kwa kuwa isingehitajika sana kukuomba Wewe chochote bila—bila kukifanyia kazi, kuadini ya kwamba Wewe—ya kwamba Wewe utakifanya. Tutangojea kwa matarajio ya kwamba Wewe utatujalia.

⁶³ Ndipo ibada zitakapofungwa Jumapili ijayo alasiri, jalia kuwe na lundo la viti vya magurudumu hapa pembeni, vitanda vya wagonjwa, machela, jalia kuwe na wenye dhambi walioosha katika Damu ya Mwana-Kondoo huku wameinua mikono yao hewani, wakimsifu Mungu. Jalia makasisi, wachungaji Wako wa thamani, wanaowalisha kondoo Wako, mioyo yao na iwake moto sana hata wapewe huduma mpya. Tujalie, Bwana. Bariki kila kanisa na kila mhudumu kote nchini, kila mtakatifu, na umwokoe mwenye dhambi.

⁶⁴ Tunapolikaribia Neno Lako sasa, kwa ajili ya msingi mdogo tu wa kuanzisha mkutano, usiku wa leo, tunaomba ya kwamba utalibariki. Tunajua ya kwamba maneno yetu yatashindwa, bali Maneno Yako hayawezi kushindwa, kwa hiyo tunapolisoma Neno Lako, tunaomba ya kwamba utatufasiria kwa Roho Mtakatifu. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu, kwa ajili Yake. Amina.

⁶⁵ Sasa, msisahau sasa, pigeni simu, mahali fulani, watoeni wagonjwa, wale ambao kweli ni wahitaji, nazo kadi za maombi zitasambazwa. Sasa, hu—huna budi kupata kadi ya maombi, itakuwa na namba juu yake, herufi na namba.

⁶⁶ Kila jioni kadi hizo za maombi zitasambazwa, na, kuanzia saa kumi na mbili u nusu hadi saa moja na nusu, ndipo basi, wataitwa kwa namba hizo. Hiyo ni kuwazuia watu wasikimbie, wala si uwanja wa michezo, mwajua, ni—ni kanisa, na lazima lifanywe kwa utaratibu, na kama Paulo alivyosema, “Kwa adabu

na kwa utaratibu.” Na kwa hiyo, tunawataka waje tu wakati namba zao zinapoitwa, wapate kuhudumiwa jukwaani.

⁶⁷ Sasa, hizi kadi za maombi haziwezi kubadilishwa, inakubidi kuitunza kadi yako mwenyewe. Huwezi kuichukua, umpe jirani, kumleta jirani, huyo jirani anapaswa kuja asikie maagizo kusudi apewe kadi. Kama . . . Maana mara nyingi namna hiyo, ukiwaleta watu kwenye mstari wa maombi wasiojua lolote kumhusu Mungu, basi wewe huyo hapo tena, unaona. Na—na kwa hiyo acheni waje wasikie maagizo, na kujenga imani yao wenyewe kufikia mahali pa kupokea uponyaji wao tunapowaombea wagonjwa. Hiyo itakuwa kesho alasiri, sasa, kati ya saa kumi na mbili u nusu na saa moja na nusu.

⁶⁸ Ningependa kusoma kutoka Luka Mtakatifu mlango wa 2, kifungu cha 25 na cha 26:

Na tazama, pale Yerusalemu palikuwa na mtu, jina lake Simeoni; . . . naye ni . . . mwenye haki, mcha Mungu, akiitarajia faraja ya Israeli: na Roho Mtakatifu alikuwa juu yake.

Naye alikuwa ameonywa na Roho Mtakatifu, ya kwamba hataona mauti kabla ya kumwona Kristo wa Bwana.

⁶⁹ Ningependa kutumia kwa ajili ya muktadha, ama, kwa ajili ya somo hapo kujenga muktadha juu yake, *Matarajio*. Sasa, mikutano kama hiyo huleta matarajio. Na—na unapooni jambo lisilo la kawaida likiendelea . . . Kwa kawaida tuna matabaka matatu ya watu wanaohudhuria ibada hizo, kama ilivyokuwa katika siku za Bwana wetu, na wakati wote, kuna asiyeamini, anayejifanya mwaminio, na mwaminio. Inavutia tu usikivu huo, imekuwa hivyo daima.

⁷⁰ Lakini *matarajio*, hilo ni jambo kubwa, kutarajia jambo fulani, kwa kawaida unapata kile unachotarajia. Baadhi ya watu huja mkutanoni na kusema, “Vema, si—sikutarajia kupata chochote kutoka kwake.” Vema, hawatapata, bali wale wanaotarajia kupata kitu, Mungu atawapa matarajio yao, kama wanafanya hivyo kwa uchaji na katika kumcha Mungu.

⁷¹ Sasa, sikuzote kutafuta kujua jambo fulani, kwanza ni kuchunguza kama ni mapenzi ya Mungu au la. Na halafu kama ni mapenzi ya Mungu, basi kusudi lako kwake, na halafu nia yako katika kulitekeleza, kama ni mapenzi ya Mungu, na kusudi lako ni sahihi, na nia yako ni nzuri, halina budi kutukia, hakuna njia kabisa ya kulizuia lisitendeke.

⁷² Kwa hiyo, kwanza tafuta mapenzi, kama ni mapenzi ya Mungu, na halafu, una lengo gani katika kufanya jambo hilo? Nini . . . ? Kama ni ubinafsi, ka—kamwe huta—huta—hutafanikiwa, hivyo tu. Halina budi kuwa safi kabisa na dhahiri mbele za Mungu, la siyoy halitatukia, hivyo tu. Ni, daima huna budi kuweka hilo niani mwako, ya kwamba halina budi kuwa

safi na dhahiri, mikato yako lazima iwe safi na dhahiri mbele za Mungu, la sivyo Mungu hawezi kufanya kazi pamoja nawe.

⁷³ Sasa, watu wa nyakati zote daima, ambao wamemsikia Mungu... Na popote alipo Mungu, mambo ya kimbinguni yapo, kwa sababu Yeye ni Mungu wa kimbinguni akifanya mambo ya kimbinguni. Mnaamini hilo?

⁷⁴ Sasa, katika Agano la Kale walikuwa na njia ya kujua kama ujumbe ulikuwa wa kweli au la. Sasa, chini ya ukuhani wa Walawi walikuwa na kile walichokiita *Urimu na Thumimu*, na hicho kilikuwa ni kifuniko cha kifuani ambacho Haruni alikuwa nacho hapa, alikuwa na yale mawe kumi na mawili ya kikabila kwenye kile kifuniko cha kifuani. Nao wakakitundika hicho pembeni, ama, kwenye nguzo hekaluni, halafu basi, wakati nabii alipotabiri, ama mwotaji akasimulia ndoto yake, basi wakati alipokuwa akiisimulia, kama Nuru hizo zitafanyika mkusanyiko wa Nuru, kama upinde wa mvua unaoakisi kutoka kwenye Urimu na Thumimu hiyo, ilikuwa ikionyesha ya kwamba mambo ya kimbinguni yalikuwako, basi nabii huyo alikuwa akisema kweli, ama ndoto ya mwotaji huyo ilikuwa ni ya kweli.

⁷⁵ Hata hivyo, haidhuru ilisikika halisi jinsi gani, sasa kumbukeni hili, haidhuru ilisikika halisi jinsi gani, kama Urimu na Thumimu hiyo haikutoa Nuru ya kimbinguni, wasingeweza kuipokea, kwa sababu haikuwa ni Mungu. Kwa hiyo unapomwona mtu yeyote akihubiri Injili ambapo Mungu hashuki na kuthibitisha hilo kwamba ni kweli, wewe achana nayo, maana si sahihi.

⁷⁶ Mungu angali anabaki Mungu, Yeye yu hai leo, Yeye yu hai kadiri alivyowahi kuwa, Yeye—Yeye ni Mungu. Sasa, sasa, wakati huo ukuhani ulipoondolewa, ndipo tukapata ule ukuhani mpya, na sasa, kuna Urimu na Thumimu m—m—mpya, hiyo pia, pamoja na ukuhani huu, na hiyo ni Neno la Mungu; Neno la Mungu ni Urimu na Thumimu ya Mungu. Basi kama Mungu akiahidi jambo lolote katika Biblia, nawe unaweza kulikubali kwa moyo wako wote na kuamini kwamba ndivyo lilivyo, utaona mambo ya kimbinguni ya Neno la Mungu yakitukia na kudhihirisha jambo ambalo umeaminia, haidhuru ni nini, kama unaamini.

⁷⁷ Neno la Mungu ni Mbegu, linapandwa katika moyo wa mwanadamu, na kama hakuna kitu mle cha—cha kulizua, kama tu vile, Mungu anapofanya uamuzi, ndio uamuzi Wake wa mwisho, na iwapo wewe una uamuzi wa mwisho, na wa Mungu ni vile vile tu, wakati hayo mawili yanapokutana, jambo fulani halina budi kutukia, kamwe haliwezi kuzuilika lisitukie. Unaona? Wakati uamuzi wako wa mwisho ni sawa na wa Mungu, basi jambo fulani halina budi kutukia.

⁷⁸ Mungu anapotoa tamshi, halina budi kuwa hivyo, basi unapochukua msimamo wako kwamba hiyo ni kweli, jambo

fulani halina budi kutukia, ni ninii tu, halina budi kutukia. Nao watu katika nyakati zote wakati wamesikia Sauti ya Mungu ikisema nao, wame—wameona mambo ya kimbinguni, nao wametarajia na kuishi maisha yao wakitarajia jambo hili kutukia nalo kamwe halikushindwa kamwe.

⁷⁹ Ibrahimu alimtarajia mtoto huyo mchanga kuja, hata kuendelea mpaka miaka ishirini na mitano baada ya huyo kuahidiwa kwake, alikuwa angali anamtarajia, vivyo hivyo tu wakati alipokuwa na umri wa miaka mia moja, kama alivyofanya wakati ahadi ilipotolewa kwenye umri wa miaka sabini na mitano. Nayo Biblia ilisema ya kwamba hakuwa mnyonge kamwe, bali alizidi kupata nguvu wakati wote, akiamini ya kwamba Mungu angeitimiza.

⁸⁰ Mngeweza kuwazia mzee sasa, mwenye umri wa miaka sabini na mitano, na mwa—mwanamke wa sitini na mitano, mke alikuwa tasa na mume alikuwa mgumba, nao hawa hapa wakitoka nje sasa, wakishuka kwenda kwa daktari hospitalini kufanya maandalizi kwa ajili ya kitanda, watapata mtoto? Naam, mwanamke mwenye umri wa miaka sitini na mitano na mwanamume wa miaka sabini na mitano. Daktari huyo angesema nini? “Maskini huyo mume na mke wakongwe kidogo wamerukwa na akili.”

⁸¹ Vema sasa, mtu yeyote ambaye kweli analiamini Neno la Mungu vile vile lisemavyo anahesabiwa kidogo amerukwa na akili, kwa sababu ninii, Hilo ni la kimbinguni sana ulimwengu wa kawaida haujui chochote juu Yake, wao ni . . . Ni upumbavu kwa watu wa kimwili, kwa hiyo kamwe hutalielewa.

⁸² Lakini Ibrahimu aliliamini, akasema, “Ni kweli,” naye aliamini lilikuwa ni kweli. Sasa ninaweza kumsikia kama vile angemwambia Sara, “Sasa tutapata mtoto huyu, Mpenzi. Imetatuliwa, kwa sababu Mungu alisema hivyo.”

⁸³ Akanunua jicho ndege, na pini, na kuandaa kila kitu, akatengeneza vijibuti, na alikuwa tayari kabisa. Na baada ya siku *kadha* za kwanza, siku ishirini na nane, “Unajisikiaje, Mpenzi?”

“Hakuna tofauti, Mpenzi.”

“Mungu asifiwe, tutampata kwa vyovyote vile.”

⁸⁴ Mwezi wa kwanza ukapita, hakuna tofauti, mwezi wa pili, mwaka wa kwanza, mwaka wa pili, “Unajisikiaje, Mpenzi?”

“Hakuna tofauti.”

“Utukufu kwa Mungu, utakuwa mwujiza mkubwa kuliko ilivyokuwa miaka miwili iliyopita, ni mkubwa zaidi kwa miaka miwili sasa.”

⁸⁵ Na wakati miaka ishirini na mitano ilipopita, angali alikuwa na msimamo ule ule, vile vile tu, kwa sababu Mungu alisema hivyo.

“Unajuaaje?”

⁸⁶ “Mungu alisema hivyo, hilo latosha. Kama Mungu alisema hivyo, hilo, hakuna la zaidi la kusema juu yake, mnaona, Yeye alisema hivyo.” Na akiwa na umri wa miaka mia moja angali alimwamini Mungu, kwamba Mungu angefanya hivyo.

⁸⁷ Biblia ilisema katika Waebrania 4 ya kwamba Ibrahimu hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alikuwa na nguvu, akimtukuza Mungu. Nasi tunapaswa kuwa Uzao wa Ibrahimu, “Kwa kuwa sisi tuliokufa katika Kristo tu Uzao wa Ibrahimu.” Hiyo ni kweli? Roho Mtakatifu anatufanya Uzao wa Ibrahimu. Ibrahimu hakuwa Myahudi, Ibrahimu alikuwa Mmataifa, bali haikuwa ni Myahudi wala Mmataifa, imani yake katika Neno la Mungu ndiyo iliyomfanya ku—kuwa mrithi wa ile ahadi. Nasi tukiwa tumekufa katika Kristo ni Uzao wa Ibrahimu, nasi ni warithi pamoja Naye, kulingana na ahadi.

⁸⁸ Ninawaambia hiyo ni kweli ndivyo tulivyo, lakini wakati mwingine hatutendi hivyo. Wakati mwingine tunaenda na kusema, “Vema, nitaenda na kuombewa, nami nitaona kitakachotukia. Vema, sijisikii tofauti hata kidogo.” Ati uzao wa Ibrahimu? Loo, jamani! Hicho ni kisingizio duni kwa, hata kwa mshiriki wa kanisa, sembuse kuwa Uzao wa Ibrahimu. Uzao wa Ibrahimu hauangalii hali yoyote ya mambo, unaangalia Neno la Mungu, hivyo tu.

⁸⁹ Hapa wakati fulani uliopita niliitwa kando ya kitanda, yapata miaka kumi iliyopita, kwa nanii, vema, imekuwa yapata miaka kumi na miwili iliyopita sasa, kwa mvulana anayekufa, akifa kwa dondakoo nyeusi. Naye daktari asingeniruhusu niingie, alisema, “Siwezi kukuruhusu uingie, wewe ni mtu aliyeoa.”

⁹⁰ Naye huyo daktari alikuwa Mkatoliki, mwenyewe, basi nikasema, “Sasa, kama kuhani alikuja, naye mvulana huyu alikuwa anakufia humu ndani, nawe ulijua na kusema atakufa usiku wa leo, nawe. . . ungemruhusu huyo kasisi aingie?”

Kasema, “Bila shaka.”

“Ampe kaida za mwisho?”

“Naam, bwana.”

Nami ni—nilijua angempa, asili yangu ni Katoliki, pia, kwa hiyo nikasema. . . Ni—ni—nilijua angefanya hivyo. Nikasema, “Vema, sasa. . .”

Akasema, “Naam, lakini yeye—yeye si mtu aliyeoa, wewe una watoto, ungebeba huu na kuwaambukiza watoto, una watoto wawili wadogo.”

Nikasema, “Naam, bwana, hiyo ni kweli.” Lakini nikasema, “Imani yangu katika Mungu. . .”

Akasema, “Ah, uh, toka nje.” Mnaona?

⁹¹ Nami nikasema, “Vema sasa, angalia, hiyo... Mi—mimi ni vivyo hivyo tu kwa mvulana yule mle ndani, kulingana na huyu baba na mama wanaosimama hapa, kadiri ya vile kasisi angekuwa kwako kama ulikuwa unakufa namna hiyo,” unaona, nikasema, “vivyo hivyo tu. Imani yetu inamtazama Mungu vivyo hivyo.”

⁹² Hatimaye, akanivalisha kama Ku Klux, kisha akaniruhusu kuingia. Kwa hiyo ni—nikaenda kumwomba huyo mvulana, naye huyo mvulana alikuwa pale, basi maskini nesi mmoja akaambatana nasi, maskini baba na mama wakapiga magoti upande wa pili wa kitanda. Walikuwa naye, wakivuta ninii yake, hewa ndani yake huku na huko, na upumuaji bandia. Nao wakasema, wao... .

⁹³ Nikapiga magoti na kuomba, ombi dogo tu la kawaida, nikaweka mikono juu ya huyo mvulana, nikasema, “Sasa, Bwana, Wewe uliahidi ya kwamba ungefanya jambo hili, huyu baba na mama wanaamini hili, kwa hiyo ninaweka mikono yangu juu ya huyo mvulana, Nawe ulisema ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa watapata afya, kwa hiyo, Bwana, moyoni mwangu ninaamini ya kwamba Wewe hutimiza Neno Lako, na vivyo hivyo huyu baba na mama. Imekwisha, Baba. Asante.” Nikasimama.

⁹⁴ Ndipo maskini huyo baba akamshika huyo mama upesi, naye mama akamshika baba wakaanza kukumbatiana, na kulia tu, kasema, “Si ni ajabu, Mpenzi? Si ni ajabu?” Wala huyo mvulana hakusogea kamwe, alikuwa amepoteza fahamu kwa siku mbili au tatu. Kisha kasema, “Loo, si ni ajabu?”

⁹⁵ Ndipo nikasema, “Bwana awabariki nyote,” kisha nikaanza kutoka nje. Maskini... Nami nikatoka nje, nao waka... wakinisindikiza huko nje kusudi niweze kuendelea.

⁹⁶ Kwa hiyo basi, maskini huyo nesi akaja, akasema, “Bwana,” akasema, “Kamwe siwezi kuelewa,” alikuwa tu ni msichana, kasema, “Siwezi kuelewa. Mnaona,” namna fulani ya kadiogramu, kitu fulani ambacho... kasema, “kama hiyo ikiwahi kushuka mahali fulani,” kasema, “historia yote, haijajulikana kamwe kupanda tena,” kisha kasema, “jambo pekee linalomweka mvulana huyo hapa; anadhoofika wakati wote,” kasema, “yeye yuafa tu—yuafa tu sasa hivi.” Kisha kasema, “Wakati yeye, mtu huyo alipofanya maombi hayo kwa ajili ya mtoto huyo mchanga, ama, mvulana huyo,” kasema, yeye ana umri wa kama miaka kumi na miwili, kumi na minne, kasema, “Wewe...” Kasema, “Haikumbadilisha hata kidogo,” kasema, “hajabadilika hata kidogo.” Kisha kasema, “Sindano hiyo ingali inaning’inia papa hapa chini,” kasema, “yeye ni kama tu alivyokuwa.” Kisha kasema, “Haiwezi kupanda tena, kwa sababu imeshuka, na ni hivyo tu.”

⁹⁷ Ndipo maskini yule mzee muungwana, mwajua, kama baba, akamkumbatia maskini huyo nesi, naye akasema, “Loo, mtoto wangu wa thamani.” Akasema, “Bwana akubariki, kipenzi.” Akasema, “Sitaki kukudhihaki, kwa sababu...wala nisingepinga yale usemayo,” akasema, “lakini, unaona,” kasema, “umefunzwa kuamini kwamba wakati sindano hiyo, ama mkono, ama chochote kile kinaposhuka huko chini, kwamba hakiwezi kurudi tena.”

⁹⁸ Akasema, “Bwana, hiyo ni kweli,” akasema, “ha—haiwezi kurudi tena.” Kasema, “Mvulana huyo amekwisha.” Kasema, “Yuko hapa kwa shida.” Kisha kasema, “Yeye, ukiondoa hii kwake, angekufa sasa hivi.”

Akasema, “Mpenzi,” akasema, “Unaangalia sindano hiyo.”

Kasema, “Kweli kabisa.”

Yeye—yeye alikuwa ndiyo kwanza amwulize, kasema, “Unawezaje kucheka na kuendelea namna hiyo, huku mvulana wako anakufa?”

Akasema, “Hafi,” kasema, “ameponywa.”

Kisha kasema, “Vema, unawezaje kutarajia hiyo huku sindano hiyo...?”

Kasema, “Mpenzi, hiyo tu ndiyo unayojua kuangalia, ni hiyo sindano, bali ninaangalia ahadi,” hiyo ni kweli, “ambayo Mungu alifanya.”

⁹⁹ Naye mvulana huyo ana watoto wawili, naye yuko Afrika leo hii, mmishenari. Loo, inategemea kile unachoangali... Alikuwa *akitarajia* hilo litukie, kwa sababu alikuwa ametimiza masharti ya Mungu, mnaona. Akamweka huyo mvulana madhabahuni, alikuwa, sayansi ya tiba ilikuwa imefanya yote waliyoweza kufanya, kila kitu kilikuwa kimepita msaada wowote wa kimwili ambao huyo mvulana angeweza kupewa, kwa hiyo akamjia Mungu na kuamini ya kwamba Mungu angemfanyia...Nayo Biblia ilisema, “Yeye huwapa thawabu wale wamtafutao kwa bidii.” Hiyo ni kweli.

¹⁰⁰ Wewe mtafute kwa moyo wako wote na umaanishe, Mungu atakuwa hapo kukutana nawe. Hiyo ni kweli. Lakini haikubidi kuzembea, inakupasa kumjia Mungu moja kwa moja, na kukiri kila kitu, na kukiweka wazi, kisha uje kwa misingi hiyo, na Mungu atakutana nawe huko, Naye atakufanyia kitu, atayajibu maombi yako.

¹⁰¹ Kila mtu aliyewahi kumwamini Mungu, ama kuisikia Sauti ya Mungu, alimtarajia Yeye afanye jambo fulani. Mungu aliponena na Nuhu katika Agano la Kale, sasa, hakukuwa kumewahi kuwako na mvua yoyote duniani. Mbona kuna...Mungu aliinyunyizia dunia maji kote, kabla ya yale maangamizi yaliyotangulia gharika, mbona, Yeye alitia maji kwa umwagiliaji, kote duniani, haikuwa imewahi kunyesha.

¹⁰² Ndipo Mungu akanena na—na Nuhu na kumwambia atengeneze safina kwa ajili ya kuokolewa kwa nyumba yake, kwamba ilikuwa inaenda kunyesha, mvua ilikuwa inaenda kuja kutoka angani, na dunia nzima itafunikwa na maji, naye Nuhu alikuwa akitarajia jambo hilo litukie. Kama asingalitarajia jambo hilo, mkosoaji wa kwanza aliyekuja, angalisema, “Vema, nadhani labda nilikosea, haikuwa Mungu.” Mnaona? Kwa hiyo angeondoka.

¹⁰³ Sasa, hivyo karibu ndivyo toleo la 1961 la kanisa lingetenda. Lakini hiyo kweli si... Mkristo halisi aliyezaliwa mara ya pili, Mungu anaposema hivyo, tunatarajia iwe hivyo, Mungu alilisema, na hivyo ndivyo litakavyokuwa, halina budi kuwa hivyo.

¹⁰⁴ Yeye alisema... Mwajua, kwa nini tuko hivyo, kwa nini tuko jinsi tulivyo siku hizi, jinsi kanisa lilivyo vuguvugu katika Wakati huu wa Kanisa la Laodikia? Mbona, ni, Mungu alisema ingekuwa hivyo, huwezi kutarajia kitu kingine, haina budi kuwa hivyo, hiyo ni kweli. Lakini Yeye ana... “Wote awapendao Yeye huwarudi na kuwakemea.” Na, “Nasimama mlangoni nabisha, na kama mtu yeyote angeisikia Sauti Yangu,” hiyo ndiyo hotuba kwa wakati huu wa kanisa, ya Mungu katika Biblia ya Ufunuo mlango wa 3 kwa Wakati wa Kanisa la Laodikia.

¹⁰⁵ Sasa, tunaona ya kwamba Nuhu alikuwa, alijitengenezea safina, akiongozwa na hofu na kutengeneza safina, akasimama hapo mlangoni akiwahubiria wasioamini, bali alikuwa akimtarajia Mungu kutimiza ahadi Yake, kwa sababu alikuwa ameisikia Sauti ya Mungu ikimwambia kwamba ilikuwa inaenda kunyesha.

¹⁰⁶ Sasa, kama unaweza kuketi papo hapo ulipo sasa na *hivyo* kujiweka wakfu kwa Mungu na kumtarajia Mungu kufanya jambo fulani, kuisikia Sauti ya Mungu ikinong’oneza moyoni mwako, “Haikubidi kungojea kadi ya maombi kesho usiku, *huu* ndio wakati nitakapokuponya,” hivyo tu, imekwisha, kusingekuwa na kitu chochote kingeweza kukutikisa kutoka hapo.

¹⁰⁷ Kama hujawahi kumpokea Roho Mtakatifu, nawe unasema, “Bwana, nimemtafuta Roho Mtakatifu kwa miaka kadhaa, lakini ndio kwanza nisikie Sauti ikiniambia nitampata, usiku uu huu,” hilo latosha, hilo—hilo ndilo, utakuwa ukitarajia *sana*, itabidi litendeke.

¹⁰⁸ Sasa, Nuhu alikuwa, alisimama pale akiigongagonga safina hiyo, kwa sababu alikuwa akitarajia kunyeshe.

¹⁰⁹ Sasa, hebu na tuchukue tu muda kidogo na tuwaone wakosoaji wakija na kusema, “Vema, sasa hebu kidogo, bwana. Bw. Nuhu, unaniambia itanyesha.”

“Naam, bwana.”

¹¹⁰ “Sasa, mimi ni mwanasayansi.” Ambapo walikuwa na wanasayansi. Wanasayansi walikuja kupitia kundi la Kaini. Kwa hiyo akasema, “Sasa, sisi—sisi ni wanasayansi, na—na tungetaka utuonyeshe mahali mvua hiyo ilipo *huko juu*.”

¹¹¹ Sasa, imani si kile unachoweza kuona, bali ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. Mungu alisema hivyo, haitubidi kuthibitisha chochote. Kuthibitisha si kitu, huwezi kumthibitisha Mungu. Hata huwezi kuthibitisha una akili. Hiyo ni kweli. Huwezi kufanya hivyo. Kama ukinijalia kukiona, kukionja, kukihisi, kukinusa, ama kukisikia. Uliwahi kuhisi nia yako, kuona nia yako, kuonja nia yako? Unaona, hisi hazitaitangaza, bali hata hivyo unayo, unajua unayo.

¹¹² Na hivyo ndivyo tu ilivyo kwa Mungu. Unasema, “Ninajuaje nina nia?” Ninaona jinsi ninavyotenda. Ninajua jinsi *Kitu fulani* kilivyonibadilisha kutoka mwenye dhambi nikawa Mkristo, ninaye Mungu ambaye ninajua kwamba—kwamba ni—kwamba ni halisi, halisi tu kadiri akili yako ilivyo halisi, ama—ama—ama hisi nyingine yoyote ambayo ingefanya kazi.

¹¹³ Sasa, angalieni, kuna hisi tano tunazolingilia katika mwili wa mwanadamu, hisi tano. Nafsi ina milango mitano, pia, ambayo ni, dhamiri, na kadhalika, na mawazo, lakini kuna mlango mmoja tu wa roho (huo ni nafsi, mwili, na roho), kwa roho, na hiyo ni kupitia njia ya hiari, ambalo linamweka kila mwanamume na kila mwanamke kwenye msingi ule ule uliokuwa katika bustani ya Edeni.

¹¹⁴ Unataka kufanya...una ninii...Wewe ni mtu mwenye uhuru wa kujichagulia kutenda vyovyote utakavyo, wala hakuna moja ya hisi hizi zingine iliyo na uhusiano wowote nayo, si nafsi wala mwili, bali ni kupitia kwa roho juu ya hiari. Mungu alimwambia Adamu, “Siku utakayokula, siku hiyo utakufa.” Sasa, angeweza kula na kuishi, ama, a—angeweza—angeweza kula na kufa, ama kuachana nayo na kuishi. Hivyo ndivyo tulivyo, usiku wa leo, tunaweza kulichukua Neno Lake na kuponywa, ama tunaweza kuliacha, kuliondokea, tusiponywe. Tunaweza kuwa na Uzima wa Milele kwa kumwamini Yeye, ama tunaweza kuondoka wala tusipate Uzima wa Milele, ni juu yako, hiari yako mwenyewe.

¹¹⁵ Ndipo Nuhu aliposikia Sauti ya Mungu ikimwambia itanyesha, nayo mawingu yanakuja, nayo itanyesha, wala haijawahi kunyesha katika nyakati zote, na—na, lakini itanyesha, Nuhu alijua jambo hili, ya kwamba Mungu alikuwa ni Mungu Muumba, ya kwamba Yeye angeweza—Yeye angeweza kufanya lolote alilotaka kufanya, na kwa hiyo, Ye—Yeye alikuwa ni Mungu wala hakukuwa na kitu kingine chochote kwake, alijua tu ya kwamba—ya kwamba Yeye aliweza kutengeneza

mvua huko juu, kama hakukuwako na yoyote kule juu. Yeye ni *Yehova-Yire*, “Bwana alijitolea Mwenyewe dhabihu.”

¹¹⁶ Kwa hiyo Mungu anaweza kutengeneza mvua, kama hakuna mawingu huko juu, hakuna mvua huko juu, kama Yeye alisema itanyesha, Nuhu alisema, “Nitajenga tu safina hii sasa hivi haidhuru,” kwa kuwa alikuwa akitarajia kunyeshe. Na wakati alipojenga ile safina, kila kitu kilikuwa katika utaratibu, ilinyesha kwa sababu alikuwa anaamini. Sasa, inakufanya utende kigeni wakati u—unapoliamini Neno la Mungu kweli, na wakati unatenda kana kwamba unalitarajia.

Nimeona watu wakija, jukwaani, wakasema, “Vema, angalia, mimi ni mgonjwa, jamani. Hivi hujui?”

“Mbona, hakika ninajua wewe ni mgonjwa.” Vema.

“Vema, unaweza kufanya jambo fulani?”

¹¹⁷ Mbona, kamwe hu—hutaupata namna hiyo. La, bwana. Nanyi mtawaombea, mwawekee mikono, wataondoka jukwaani, “Sijisikii tofauti hata kidogo.” Huh, hutajisikia, hilo ni jambo moja la hakika, hutajisikia. Sasa, hukuwa ukitarajia chochote.

¹¹⁸ Wewe njoo jukwaani na kufuata maagizo ya Mungu jinsi tu asemavyo Mungu, kisha uondoke, ukiwa na matarajio, “Naam, bwana, nitaupokea. Tayari imefanyika! Nilifanya yale Mungu aliyoniambia nifanye, kwa hiyo hilo latosha.” Hivyo—hivyo ndivyo, huyo ni Uzao wa Ibrahimu.

¹¹⁹ Sasa, tutachukua mwingine: Musa. Musa, loo, yeye alikuwa ni mwanatheolojia aliyefunzwa, kweli alijua, maana angeweza—angeweza kuwafundisha Wamisri hekima; alikuwa mwerevu sana. Naye alijua ya kwamba alizaliwa, akalelewa kuwa mkombozi wa Israeli, kwa hiyo alifikiri angeweza kuchukua mafunzo yake ya kitheolojia na kweli aende huko nje na kufanya hivyo, lakini akaona kwamba alikuwa ameshindwa.

¹²⁰ Na tunapojaribu kulielimisha kanisa lipate ushirika, tunapojaribu kuwaelimisha watu kwa Kristo, tunapiga tu hewa, kamwe hatutafika popote. Kuna njia moja tu ambayo mwanamume au mwanamke anaweza kumjia Kristo, hiyo ni kupitia kwa Damu ya Yesu Kristo kwa kuzaliwa mara ya pili, hiyo ndiyo njia pekee tunayoweza kutembelea. Unapoingia kwenye hiyo, basi unapokea imani halisi, ya Roho Mtakatifu hiyo inakufanya kuita chochote kinyume na ahadi ya Mungu kana kwamba hakikuwepo.

¹²¹ Haidhuru hali ya mambo ikoje, jinsi ulivyo mgonjwa, yale daktari aliyosema, alikukatia tamaa, utakufa kwa kansa, una ugonjwa wa moyo, huenda ukaondoka dakika yoyote, hata huangalii hilo, unaangalia yale Mungu aliyosema. Dumu papo hapo juu ya yale Mungu aliyosema, kwamba, Yeye alisema hayo, na hilo latosha wakati wote. Sasa, huwezi kulidanganyia, huna budi kuliadini kweli.

¹²² Kama ukisema, “Loo, naam, ninaliamini...” Loo, nimeona watu wakisema hivyo, na kama imani ilikuwa ni wino, wasingeweza kutonesha *i*, walininii tu—kwa urahisi tu, wamesisimkwa tu, ni tumaini badala ya imani. Imani halisi haichukui *la* kama jibu, ina—ina nywele kifuani, ni kubwa na nene, inazungumza na kila kitu kinaketi chini, hivyo tu.

Kama maskini, mnajua, hisia zinainuka, kasema, “Hu—husikii tofauti yoyote. Wewe unaninii tu...”

Atasema, “Nyamaza!” Imani itasema. “Keti chini, Mungu alichukua mamlaka.” Jambo ndilo hilo. Sasa, ni ninii...

“Vema, tumbo lako bado linauma.”

¹²³ “Nyamaza! Hata siuhisi.” Jambo ndilo hilo. Hiyo ni... Usi—usiwe... Hakika, ni kuangalia yale Mungu aliyosema. Mungu alisema hivyo, kwa hiyo imani huliamini. Kama unaweza tu kushikilia imani kwako, kwamba... iache tu imani itawale, inawafanya hao wengine waonekane tu kama maskini vibushuti. Inawafanya tu waketi chini kwa sababu yeye ndiye bosi, ana misuli mikubwa mno, migumu, nami nawaambia, kila kitu kingine hisia zote, na ushirikina, na *itikadi* ndogondogo, na kadhalika, huketi tu chini wakati imani inapochukua mamlaka, ananinii tu, yeye ndiye bosi. Hiyo ni kweli.

¹²⁴ Sasa, nanyi ni... Bila shaka, Musa alidhani alikuwa na hiyo. Lakini wakati alipoingia kwa njia yake mwenyewe na kugundua kwamba alifanya kosa, kisha akarudi na kumwoa maskini mwanamke Mkushi, mrembo, akamzaa mwana huko nyuma, Gershomu, naye alikuwa ametulia kwenye maisha mazuri ya kuwafuga kondoo, naye alijua ya kwamba angekuwa mrithi, mara tu Yethro alipokufa angeirithi mifugo hao wote mwenyewe, na kwa hiyo alikuwa ameridhika sana.

¹²⁵ Lakini siku moja alikuwa akirudi upande wa nyuma ya jangwa, kulikuwa na jambo fulani lililotukia ambalo kamwe halikutokea katika seminari, kulikuwa na jambo lililotukia ambalo hajawahi kulisikia hapo kabla, aliona kichaka kikiwaka moto. Akaenda kando aone ilikuwa ni kitu gani, ndipo Sauti ikanena kutoka mle, ikasema, “Vua viatu vyako, Musa, mahali unaposimama ni patakatifu.” Loo, jamani! “Nimesikia vilio vya watu Wangu, nimeona mateso yao. Ninakumbuka Neno Langu, ninakumbuka yale niliyomwambia Ibrahimu, lakini vile uzao wake utakaa kwa muda wa miaka mia nne katika nchi ya kigeni, wakati huo umekwisha, ninakumbuka Neno Langu. Vema, Musa, ninakutuma ushuke huko.”

¹²⁶ Ungeweza kuwazia mtu aliye mwoga sana hata akalitoroka taifa, aliingia katika shida kwa kumwua mtu mmoja na kulitoroka taifa, akashuka akarudi chini ya nguvu za Mungu na kuliua taifa zima, hakupata shida? Mnaona? Inaonyesha kama unalifanya katika mapenzi ya Mungu, ama huko nje katika mapenzi yako mwenyewe. Unaona? Yale unayoweza kufanya

na uingie katika shida mwenyewe, kwa nini usiachilie tu na kumwacha Mungu alifanye? Hiyo—hiyo ndiyo njia ya kulifanya.

¹²⁷ Kwa hiyo huyu hapa kesho yake, nena kuhusu jambo la kimapinduzi, unaweza kumwona Musa kesho yake, sasa, baada ya kuwa mzee mchunga kondoo, alikuwa—alikuwa na umri wa miaka themanini, labda alikuwa na ndevu ndefu nyeupe, na kichwa chenye upara, na—na alikuwa na maskini fimbo iliyopinda mkononi mwake pamoja na nyumbu, huku mke wake ameketi kwa kutagaa juu yake, akiwa na mtoto nyongani mwake, na huyu hapa anashuka chini namna *hii* akipiga mayowe tu na kupaza sauti, akishuka chini, “Utukufu kwa Mungu,” akishuka kwenda Misri.

“Unaenda wapi, Musa?”

“Nashuka kwenda Misri kuiteka.” Naam, bwana.

“Ati nini? Uvamizi wa mtu mmoja?”

“Naam, bwana. Hiyo ni kweli.”

“Kwa nini? Unajuaje utaiteka?”

“Mungu alisema hivyo.” Hilo lilitosha, mnaona. “Niliisikia Sauti Yake, ninamtarajia kufanya hivyo.” Hiyo ni kweli.

¹²⁸ Alionekana mjinga. Mtu mmoja akasema, “Maskini jamaa mzee, uvamizi wa mtu mmoja.” Akienda kama, mtu mmoja akienda kuipiga Urusi, mnaona. Lakini aliiteka, kwa sababu Mungu alisema hivyo, naye alikuwa akimtarajia Mungu kulitimiza Neno Lake. Amina.

¹²⁹ Ninamtarajia Mungu kutimizia Neno Lake nasi. Mungu atatimiza Neno Lake kwa mtu yeyote ambaye atachukua Neno Lake na kusema, “Ni langu. Mungu ametoa ahadi, nami ninakutarajia Wewe kulitekeleza. Nami sichukui *la* kama jibu, ninasimama papa hapa.”

¹³⁰ Kama vile Buddy Robinson, wakati alipokuwa akilima na maskini nyumbu wake huko nje siku moja, naye huyo nyumbu akakimbia, na kumwama sikio, naye alikuwa akijaribu kuhubiri utakaso, basi akasema, “Sasa, mimi si, mimi si ni kitu kirembo hapa chenye nywele za nyumbu kwenye meno yangu yote, huku nikihubiri utakaso?”

¹³¹ Basi, kwa hiyo akashuka kwenda hudumani, akasema, “Bwana, usiponipa Roho Mtakatifu, utakaporudi, utakuta lundo la mifupa limewekwa papa hapa, utakaporudi.” Sasa, akampokea Roho Mtakatifu, ili kwamba, hiyo baraka ya pili akaiita, utakaso.

¹³² Kwa hiyo sasa, hiyo ndiyo njia. Unapoipeleka hiyo kwa Mungu, “*Hii* ndiyo, *hii* yatosha. Mungu, Wewe ulisema hivyo, na ni hayo tu. Madaktari wamenifanyia yote wawezayo, nami ni mgonjwa asiye na matumaini mikononi mwa dawa, mimi ni mgonjwa asiye na matumaini mikononi mwa hospitali, kuna

Mmoja tu, ninajitolea mwenyewe Kwako, niko mikononi Mwako sasa. Mungu, niko mikononi Mwako.” Amina. Kaa papo hapo, jambo fulani litatukia basi.

¹³³ Jambo fulani liko karibu kutukia. Unapoisikia Sauti hiyo ya Mungu ikikwambia, “Wewe ni Wangu, ni—ninakumiliki, nilikununua kwa Damu Yangu, nitaninii...kwa kupigwa Kwangu uliponywa,” loo, ndugu, ninakwambia, jambo fulani liko karibu kutukia utakapofanya hivyo.

¹³⁴ Naam, itafanya...Loo, watu watasema, “Mbona, Lucy, Nettie, ama Martha, Mary, mbona, unajua wamerukwa na akili. Na—nawaambia, walienda kwenye mkutano kule juu, nao wakatiwa mafuta, na sasa, mwajua, tunajua alikuwa akifa kwa kansa, daktari anasema hawezi kupona, na hapa, yuko kule akifua nguo zake zote, akiimba tu, ‘Haleluya, haleluya,’ akitembea huku na huko akipiga makelelen namna *hiyo*. Mbona, maskini huyo mwanamke ameingia kichaa!”

¹³⁵ La, yeye ameamini tu Neno la Mungu. Anatenda kiwazimu kwa watu, bali anatii yale Mungu aliyosema, hiyo ni kweli, kabisa.

¹³⁶ Musa alifanya hivyo. Huyu hapa anaenda, ungeweza kuwazia, maskini jamaa huyu akichechemea kwa mguu mmoja, huyu hapa anaenda, mwajua, nyumbu nyuma yake, “Utukufu, haleluya?”

“Unaenda wapi, Musa?”

¹³⁷ “Nashuka kwenda Misri, kwenda kuiteka.” Akishuka moja kwa moja kwenda kuiteka, mwenye umri wa miaka themanini, akishuka kwenda kwenye jeshi lenye mitambo bora kuliko yote lililokuwako ulimwenguni, lilikuwa limeushinda ulimwengu mzima. Akishuka kwenda, umri wa miaka themanini, akiwa na mke na mtoto, mvulana wa—wake, Gershomu, labda ameketi kwenye nyonga yake, naye huyu hapa anashuka kwenda kule, akimwongoza maskini nyumbu huyu, akishuka kwenda ku—kuiteka, naye aliiteka. Naam. Kwa nini? Alikuwa akitarajia. Kwa nini? Mungu alisema hivyo, hilo latosha. Mungu aliposema hivyo, hiyo ilikuwa...

¹³⁸ Yohana, wakati alipotembea huko nje, naye alikuwa amesimama ukingoni mwa Yordani, amesimama akihubiri, nao makuhani kote ukingoni wakasema, “Unataka kuniambia siku itakuja ambapo dhabihu ya kila siku itaondolewa hekaluni, wala hakutakuwako na dhabihu nyingine? Wajibu umekwisha?”

Yeye alisema, “Siku itakuja ambapo Mtu mmoja atakuja, huyo atakuwa ndiye Dhabihu.”

“Loo, jirudie, Mhubiri! Kwani una shida gani? Hakutakuwako na wakati kama huo.”

¹³⁹ Ndipo akaanza kuangalia, akasema, “Tazama,” (Amina!) “tazama Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya

ulimwengu.” Kwa nini? Alikuwa akimtarajia, kwa sababu alisema, “Yeye aliyeniambia nyikani niende nikabatize kwa maji, alisema, ‘Ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu Yake, Huyu Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto, huyo Ndiye.’” Alikuwa akitarajia kumwona.

¹⁴⁰ Akasema, “Nilimjua kwa sababu kulikuwako na ishara ya Masihi juu Yake, Nuru juu Yake, ndipo nikajua huyo alikuwa ndiye Masihi.” Naye alikuwa akitarajia kumwona.

¹⁴¹ Loo, enyi kanisa, tunapaswa kuwa tukitarajia kumwona Mungu akifanya jambo fulani, tunapaswa kutarajia kuona uamsho wa mji mzima, mtikiso miongoni mwa watu, bila shaka. Tumeahidiwa, tunaamini. Ninyi aminini pamoja nami, kama tutaweke miyo yetu pamoja na kuamini, jambo fulani litatukia, halina budi kutukia. Tunalitarajia, bila shaka.

¹⁴² Loo, jinsi tungeweza kuendelea mbele, jinsi tungeweza kuendelea tu na watu mbalimbali, lakini hebu tuende kwa Simeoni sasa, katika kufunga, dakika chache zijazo.

¹⁴³ Simeoni, alikuwa ni mtu mashuhuri. Sasa, nilisoma habari zake si muda mrefu uliopita, alikuwa mahali fulani akiwa na umri wake wa miaka themanini, mzee mwenye hekima, aliyependwa sana miongoni mwa watu, bali daima alikuwa ni mtu wa kiroho. Na kwa hiyo, basi siku moja akatokea akisema, “Sitakufa, mpaka nitakapomwona Kristo wa Bwana.” Sasa, ungeweza kuwazia?

Unasema, “Unasemaje hivyo, Simeoni? Ni kitu gani kinachokufanya useme hivyo? Unaingia kichaa. Kwani umeingia kwenye *itikadi* ya aina gani?”

“Hakuna.”

“Kwa nini wewe, ni kitu gani kinachokufanya useme hivyo?”

¹⁴⁴ “Roho Mtakatifu aliniambia.” Uh-huh. “Roho Mtakatifu alinifunulia ya kwamba sitaona mauti, mpaka nitakapomwona Kristo wa Bwana, nami ninaamini hilo, hivyo tu.” Akaenda kote akimwambia kila mtu. Haidhuru jina lake lilikuwa mashuhuri jinsi gani, haikumbidi kuwa na damu ya kifalme, bali yeye alinini tu—alinini tu, sijali alikuwa nini, angali aliamini ya kwamba Roho Mtakatifu alikuwa sahihi. Vema, hakuna Roho Mtakatifu wawili, kuna Roho Mtakatifu mmoja tu. Hiyo ni kweli. Naye aliongozwa na Roho Mtakatifu, ikafunuliwa kwake na Roho Mtakatifu. Basi Roho Mtakatifu yeye yule aliyemfunulia Simeoni anaweza kukufunulia, ile ahadi aliyotoa. Hilo hapo.

Sasa, tunamwona, huyu hapa anazunguka akimwambia kila mtu, “Naam, sitakufa, si—sitakufa mpaka nitakapomwona Kristo wa Bwana.”

¹⁴⁵ Ninaweza kusikia kusanyiko likisema, “Maskini mzee Simeoni, inasikitisha sana, maskini, jamaa mzee. Mwajua, kwa

namna fulani yeye ni mdogo. . . yeye ana mguu mmoja kaburini sasa hivi, umri wa miaka themanini na kitu, tayari kufa, pia angalieni, hata huko nyuma tangu siku ya Adamu walimtazamia Kristo. Angalia, Daudi alimtazamia, aliimba juu Yake, manabii walitabiri juu Yake, na yote haya, na hapa, mzee huyu, sasa tuko mbali zaidi nalo, tulivyowahi kuwa maishani mwetu mwote, na hapa mzee huyu, akiwa na mguu mmoja kaburini, na karibu tu kuondoka, naye huyu hapa akizunguka miongoni mwa watu akisema, ‘La, sitakufa, nitamwona Kristo wa Bwana, yu karibu sana.’”

“Unajua je?”

“Roho Mtakatifu aliniambia hivyo.” Alikuwa akilitarajia, hiyo ni kweli, akitarajia litendeke.

¹⁴⁶ Vema, kama wewe—kama unatarajia litendeke, basi litatendeke. Kama tu vile nimesema mara nyingi, “Kilindi kinapoita kilindi.” Daudi alisema, “Kwa sauti ya, ya maporomoko ya maji Yako, kilindi kikiita kilindi.” Kuna jambo kuhusu *kitu fulani* unachotamani, *kitu fulani* kilicho moyoni mwako.

¹⁴⁷ Ni—ninapenda ku—kuninii. . . mandhari, na ninapenda kuwinda. Nimepanda milimani, tangu nilipokuwa mvulana mdogo, kupanda huko juu, kuangalia jua hilo likitua jioni, kuliangalia likichomoza asubuhi, kuona hilo jicho kuu la Mungu, linavyoonekana, likipitia kule.

¹⁴⁸ Angalieni majira ya kuchipua yajayo sasa, na zile mbegu ndogo zilizozikwa chini ya theluji hiyo hapa majuma machache yaliyopita, zikapasuka, zikaisha, nyama zikazitoka, hakuna kitu kilichosalia, hakuna mbegu, hakuna nyama, hakuna ubua, hakuna petali, hakuna chochote kilichosalia cha ua hilo, ni—ninii, hata mbegu, ilianguka kutoka kwake. Mnajua Mungu ana msafara wa mazishi kwa ajili ya maua Yake? Mlijua hilo? Hakika.

¹⁴⁹ Hilo dogo, jalidi hulipiga hilo ua dogo, changa au zee, linainamisha maskini kichwa chake na kufa, hayo ni mauti. Na kutoka kwenye ua hilo dogo inaanguka mbegu ndogo nyeusi ardhini, ndipo hii hapa Septemba inakuja, Oktoba inakuja basi, matone ya machozi yanaanza kuanguka kutokana na hiyo mvua ya Oktoba, mwajua, na kuizika ardhini, msafara wa mazishi. Mnaona?

¹⁵⁰ Nayo inakaa humo wakati wote wa majira ya baridi kali na kuoza, ndipo—ndipo mgando unakuja na kuipasua maskini mbegu hiyo na kuifungua, nyama yake inatoka. Nawe huenda ukachukua konzi ya hilo vumbi na kuipeleka kwenye maabara, usingeweza kuchukua kemikali yoyote ulimwenguni na kuona chembe hiyo ya uhai mle ndani, bali iko mle mahali fulani. Hiyo ni kweli. Imefichwa, huwezi kuipata, bali acha tu hi—hi—hilo jua, jua litoe uhai wote wa mimea, sasa, wakati jua hilo litakapoanza kuanguka, uhai huo utafufuka tena.

¹⁵¹ Niwaambie nini, hebu tokeni hapa nje mkaitengeneze njia yenu ya zege mwaka huu—huu, mwitengeneze tu chini uani. Basi nyasi zako ni nyingi sana wapi mwaka ujao? Ziko wapi? Ziko wapi wakati wowote? Moja kwa moja ukingoni mwa hiyo njia. Ni kwa nini? Ni uhai huo unaokaa chini ya hiyo zege, na wakati jua hilo, ingawa zimefunikwa kutoka kwake, lakini wakati jua hilo litakapoanza kuangaza, uhai huo utapenya moja kwa moja, mpaka utakapofika mwisho wa hiyo njia, na kuinua kichwa chake juu kumsifu Mungu. Kwa nini? Jua linawaka. Ndilo bwana, ndilo mtoa uhai kwa uhai wote wa mimea. Hilo, haidhuru liko wapi, litaangaza tena, uhai huo utaendelea tu kujifanyia njia, kujifanyia njia, kujifanyia njia mpaka hatimaye unatoka humo kuinua kichwa chake na kumtukuza Mungu. Basi mtu yeyote anawezaje kutoamini katika ufufuo?

¹⁵² Loo, wakati huyo, sio j-u-a la Mungu, lakini M-w-a-n-a wa Mungu, Uzima wa Milele, huenda ukanizika baharini, ungeweza kunizika chini ya chochote utakacho, lakini wakati huyo M-w-a-n-a anapoanza kuangaza katika Kuja Kwake, kila mtu aliyekufa katika Yeye na yuna Uzima wa Milele atafufuka na kwenda pamoja Naye, hakika tu kama ninavyosimama kwenye mimbara hii, usiku wa leo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...?... mara nyingi.

¹⁵³ Lakini hapa si muda mrefu uliopita, kulikuwako na m—mvulana mdogo mjini mwetu ambaye mwalimu alimwambia mama yake, kasema, “Inakubidi kumwangukia mtoto huyu, hata hivyo,” kasema, “yeye, hula tu vifutio kutoka kwenye penseli upesi kadiri tu unavyompa moja.” Akila vifutio, ndipo mama yake akamwona huko nje akila pedali kutoka kwenye baiskeli kwenye ukumbi wa nyuma, alikuwa tu na yubile ya ulaji bora, akila tu pedali kutoka kwenye baiskeli.

¹⁵⁴ Vema, wakamchukua maskini jamaa huyo na kumpeleka kwenye—kwenye kliniki wakamchunguze. Madaktari wakamchunguza, na kufanya uchunguzi wa mwili wake, ndipo wakaja kugundua, maskini jamaa huyo, mwili ulikuwa unatamani salfa. Yeye... Kuna salfa mle ndani, mwili wake ulikuwa ukililia salfa, nayo salfa iko kwenye raba, kwa hiyo hiyo ndiyo sababu alikuwa akiila hiyo raba. Sasa, kabla hapajakuwapo na kitu *hapa* cha kuitia salfa, ilibidi kwanza kuwe na salfa ya kuitikia wito huo, la sivyo kamwe kusingekuwako na wito wa salfa.

¹⁵⁵ Kwa maneno mengine, kabla hapajakuwapo na mti wa kukulia ardhini, ilibidi kuwe na ardhi kwanza mti huo upate kukulia, la sivyo kusingekuwako na mti. Kabla hapajakuwapo na samaki, pezi mgongoni mwa samaki, ilibidi kuwe na maji kwanza apate kuogelea, la sivyo kamwe asingekuwa na pezi. Mnaona? Hiyo ni kweli.

¹⁵⁶ Kwa maneno mengine, inabidi kuwe na Muumba wa

kuumba kiumbe. Na wakati, moyoni mwako...Ni wangapi wanaoamini katika uponyaji wa Kiungu? Inua mkono wako? Vema, sasa kama (Asante.), kwa hakika kadiri unavyoamini katika uponyaji wa Kiungu, kuna kitu ndani yako, ndani yako *hapa*, kinachokwambia kuna Mungu anayeponya, na kabla ya hapo, hata kabla uumbaji huo kuweza kuwa ndani yako, inabidi kuwe na Muumba wa kuumba hivyo viumbe. Amina. Jambo ndilo hilo. Sababu yenyewe ya wewe kuwa hapa usiku wa leo, sababu yenyewe kwamba mkutano huu unaendelea, inathibitisha ya kwamba kuna Chemchemi iliyofunguliwa mahali fulani ya uponyaji wa Kiungu.

¹⁵⁷ Mioyo yenye njaa, nilisimama Afrika, hivi majuzi, ambako tulikuwa na waongofu elfu thelathini alasiri moja, kaona watu ishirini na tano elfu wakiponywa kwa wakati mmoja, malori saba yaliyojaa, karibu urefu wa jengo hili, yakaondoka, kesho yake asubuhi walisimama watu ishirini na tano elfu wakitembea mitaani huku magongo yao na kila kitu kimewekwa mle ndani, na vitanda vikuukuu vya wagonjwa, na vitu walivyowabebea, wakishuka kuja. Makabila mbalimbali yakishirikiana pamoja, wakiimba, “Amini tu, mambo yote yanawezekana.” Mimi na meya wa hilo jiji tulisimama hotelini pale na kulia tu kama watoto wachanga kuona.

¹⁵⁸ Hao wenyeji waliovaa blanketi siku iliyotangulia hawakujua ni upi mkono wa kulia na wa kushoto, nao hawa hapa, Wakristo wapendwa, wameponywa kwa nguvu za Mungu katika dakika moja. Kwa nini? Waliona jambo fulani likitukia, na mara walipoliona likitukia, kitu fulani kiliwazukia, nao wakasema, “Ni mimi, pia!” Nao walipopata nafasi, waliikubali nao wakaenda zao. Hakuna lingine. Mnaona?

¹⁵⁹ Kwanza hapana budi pawe na u—uumbaji, ama, Muumba aumbe kiumbe kukufanya umtamani na kumwamini Mungu. Na inapofanya hivyo, kwa hakika kadiri unavyoamini katika hilo, hiyo inaonyesha kuna Chemchemi ya uponyaji wa Kiungu mahali fulani, hiyo ni kweli, haina budi kuwa. Nayo Biblia inanena na kusema ya kwamba ni nanii Wake, ni Roho Wake Mtakatifu anayekuongoza.

¹⁶⁰ Roho Mtakatifu yeye yule aliyemwongoza Simeoni kuamini hilo, ndiye Roho Mtakatifu yeye yule anayekuongoza kuamini katika uponyaji wa Kiungu, hakuna Roho Mtakatifu wawili, Mmoja tu. Basi Roho Mtakatifu yeye yule aliyemfunulia ya kwamba hatakufa mpaka amwone Kristo wa Bwana, Roho Mtakatifu yeye yule anazungumza nawe, “Kuna nguvu za Mungu zinazowaponya wagonjwa.” Mnaona? Loo, si ni dhahiri? Ni...Mbona, usingeweza kulifanya dhahiri zaidi. Unaona? “Kuna nguvu za Mungu zinazowaponya wagonjwa.” Mnaona?

¹⁶¹ Vema, daktari alisema, “Ninawajua hao mabwana, yeye ni...” Hilo ni sawa kabisa. Ninawaombea wakati wote, wala

simhukumu huyo daktari, la, bwana, yeye ni, yeye ni mtumishi wa Mungu, anatenda kazi juu ya watu, lakini kuna mambo ambayo hajui, na mambo fulani ambayo hawezi kufanya, basi kama hawezi kufanya, hebu tumwendee Daktari bingwa, mnaona, yule Mkuu, Mtaalamu mkuu, Tabibu mkuu, na tumwendee, Yeye, tumealikwa kuja, Yeye alituomba tuje, Yeye anatutarajia tuwepo, hiyo ni kweli, Yeye anatutarajia. Na hiyo ndiyo sababu Yeye amejifunua Mwenyewe kwako, “Mimi ndimi Bwana, niponyaye magonjwa yako yote. Mimi ni Yehova-Rafa, Yehova Mponyaji, Bwana aponyaye magonjwa yako yote.”

Kitu fulani kinakwambia moyoni mwako, “Hiyo ni kweli, ninaamini hilo.”

Vema, huyo ni Roho Mtakatifu yeye yule aliyesema, “Simeoni, hutaona mauti, mpaka utakapomwona Kristo wa Bwana.”

¹⁶² Ni wagonjwa wangapi hapa wanaoamini mtaponywa katika mkutano huu? Inua mkono wako. Sema, “Ni—ninaamini nitaponywa, wapendwa wangu, na kadhalika, wataponywa.” Vema, hilo ni sawa. Mnaona? Kitu fulani kimekufunulia hilo. Ati nini? Roho Mtakatifu yeye yule. Je, unalitarajia? Unatarajia litukie? Ni wangapi wanaoamini tutakuwa na mkutano mkuu? Inua mkono wako, useme, “Ninaamini tunaninii...” Vema. Mnaona? Nami pia. Mnaona? Ni kitu gani? Roho Mtakatifu alitufunulia. Amina. Ninaamini tutaona nguvu za Mungu. Hivi huamini hilo? Hakika. Roho Mtakatifu hutufunulia, tu—tunaamini hilo, nasi tunadumu tu moja kwa moja nalo.

¹⁶³ Sasa, mwajua, hawakuwa na televisheni siku hizo, Mungu ashukuriwe kwa hilo, kwa hiyo basi wa—wao walikuja...Ninaninii, ninaamini katika utakatifu safi, bila shaka ninauamini. Ninaamini katika...kweli, ninaninii... Mnasema...mlinisikia nikisema nilikuwa Mbaptisti muda mfupi uliopita, mimi ni Mpentekoste-Mbaptisti, Mimi ni Mbaptisti aliyempokea Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli.

¹⁶⁴ Ninaamini katika dini ya Kipentekoste ya mtindo wa kale, ya anga la bluu, inayoua dhambi. Naam, bwana. Ninaamini katika kuwa mnyofu kama mtutu wa bunduki, na kuihubiri vivyo hivyo, na kuishi jinsi tu unavyohubiri, na kuruka juu kadiri tu unavyoishi, hilo ni sawa tu. Kama huwezi kuishi juu sana, basi usiruke juu sana, bali fanya tu miruko yako sawasawa na maisha yako. Nami ninaamini ya kwamba jambo hilo linapaswa kuwa hivyo, hapo ndipo Mungu atakapoli heshimu Neno Lake, ni—ni—ni kweli ama si kweli. Nami na—naamini ya kwamba Mungu alisema, “Thibitisha mambo yote.” Nalo limethibitika kwamba ni la kweli, kwa hiyo ninaliamini. Amina.

¹⁶⁵ Sasa, angalieni jambo hili, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Sasa, si kuanza kuninii...wahudumu ndio wanaohubiri, mimi naja hapa kwa ajili ya ibada ya uponyaji, lakini nataka

kuwaulizeni jambo fulani mbele ya ustaarabu, na haki zote, na mambo ya hakika: Mnawaona wanawake wetu katika Pentekoste, na kila mahali pengine, kila mwaka wanaendelea kuvua nguo zaidi kidogo, nguo zaidi kidogo, nguo zaidi kidogo, na mpaka karibu wanakuwa, ni fedheha?

¹⁶⁶ Sasa, tunaweza kutarajia hilo kutoka kwa watu wa ulimwenguni, hawajui vinginevyo. Lakini kwa watu wetu wa Kipentekoste? Nami nawatakeni msembe kitu: Nilisimama kule ambako niliona wenyeji elfu thelathini waliovaa blanketi wakimpokea Yesu Kristo kwa wakati mmoja. Hao wanawake wamesimama pale uchi tu, walivyokuja ulimwenguni, vijana kwa wazee, bila chochote ila kitambaa kidogo, shanga zimetundikwa mbele yao kubwa *hivi*, hawakujua kamwe walikuwa uchi, hawakujua lolote kulihusu, na moja kwa moja mahali ambapo waliona uponyaji huu ukitukia, na ishara hii, ninapoiendea zaidi kesho usiku, na kuona hilo likitukia, mimi... Walitaka, walitaka kitu fulani, walitaka kumpokea Kristo. Nami nikasema, nikauliza, “Wote wanaoamini ya kwamba Yeye atawaokoa, na wasimame.” Na thelathini el... vema, waliambatanisha thelathini elfu, sijui ni wangapi waliosimama, lakini walisema thelathini elfu walisimama.

Halafu basi, ndipo Ndugu Bosworth na hao wengine wakasema, “Ninaamini Ndugu Branham, ya kwamba walimaanisha uponyaji wa kimwili.”

¹⁶⁷ Nikasema, “Sikumaanisha,” nilikuwa na wakalimani kumi na watano, mwajua, kwa hiyo nikasema, “Sikumaanisha uponyaji wa kimwili, nilimaanisha wokovu, kwamba u—umkubali Kristo, Mwana wa Mungu, kama Mwokozi wako binafsi, nawe unataka kumtumikia.” Wengi wao wakiwa na sanamu mkononi mwao, nikasema, “Ninyi mlio waaminifu kulihusu, zivunjeni sanamu zenu ardhini,” kama dhoruba ya mavumbi, mnaiona ikipanda juu namna *hiyo*.

¹⁶⁸ Na wakati, mara walipompokea Kristo, hao wanawake uchi, ndugu, dada, walikunja mikono yao namna *hii* wapate kutoka mbele za wanaume. Na kama kafiri kabisa, asiyejua mkono wa kulia na wa kushoto ni upi, mara Kristo anapowagusa, wanatambua ya kwamba wako uchi, na halafu tunadai kuwa ni wa Kanisa la Mungu aliye hai, na kujivua nguo kila mwaka, haiteti maana kwangu, kuna kasoro, mahali fulani. Hiyo ni kweli. Ee Mungu! Naam, tuko Laodikia, hapo ndipo tulipo, tuko—tuko chini kabisa mstarini karibu na Kuja kwa Bwana Yesu. Loo, hebu na tuwe tayari kumlaki. Naam, naam.

¹⁶⁹ Simeoni, kama nilivyosema, hawakuwa na televisheni. Nilipokuwa kwenye hilo, nilitoa tamshi, jambo fulani juu ya hilo wakati mmoja, kulikuwa na mama mmoja aliyeniambia, katika kuzungumza juu ya jinsi wanawake wanavyovaa maskini nguo

fupi, zinazobana, na kadhalika, na kwa hiyo akasema—kasema, “Kwa nini . . .”

¹⁷⁰ Nikasema, “Ukifanya hivyo, utawajibika kwenye Siku ya Hukumu kwa kufanya uzinzi.” Ndipo mtu fulani akaniswali juu ya hilo.

¹⁷¹ Nikasema, “Yesu alisema, ‘Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye tayari moyoni mwake.’ Nawe huenda ukawa safi kama yungiyungi kwa mumeo, ama mpenzi wako, huenda ukawa mwanamke mwenye maadili mema kama ilivyo Marekani, naam, ukiwa mwema kama ulivyokuwa ulipotoka tumboni mwa mama yako, lakini, mama, ukijivalia hivyo kuwaacha wenye dhambi wakuangalie hivyo, yeye atakutamani, na atakapofanya hivyo, kwenye Siku ya Hukumu wakati atakapowajibika kwa uzinzi wake, wewe ndiwe uliyejianika kwake, haya basi, kwa hiyo utawajibika kwa kufanya uzinzi.”

Mwanamke fulani aliniambia, kasema, “Vema, Ndugu Branham, hiyo ndiyo tu aina pekee ya nguo wanazoshona.”

¹⁷² Nikasema, “Wangali wana cherehani na wanauza vitambaa, kwa hiyo hakuna udhuru kulihusu.” Ni kile kitu tu. . . Hiyo ni kweli. Sisi, tunachohitaji leo hii, ni dini nzuri ya mtindo wa kale, ya anga la bluu, inayoua dhambi, uamsho wa kale wa Mtakatifu Paulo, na Roho Mtakatifu wa Biblia, na kuzirudia jumbe halisi za Kipentekoste tena, kurudi kwenye ile kweli.

¹⁷³ Vile ilivyo siku hizi, wainjilisti wamejaa hudumani, uninjilisti unakuwa ndio riziki kwao. Wana mipango mikubwa sana ya kudhamini, hawawezi kusema jambo hilo mbele ya kanisa. Mhudumu fulani aliniambia, kasema, “Utaiharibu huduma yako kwa hiyo.”

¹⁷⁴ Nikasema, “Huduma yoyote ambayo Neno la Mungu litaharibu, inapaswa kuharibiwa, kutupwa nje, kwa vyovyote vile.” Naam, bwana. Nikasema, “Mimi . . .” Hiyo ni kweli. Huninii. . . Tunachohitaji ni kurudi kwenye Biblia, kurudi kwenye utakatifu halisi, kumrudia Mungu, kurudi—kurudi ambapo watu wanaweza kuwa na imani. Mungu anawezaje kulijenga Kanisa Lake juu ya msingi kama huo?

¹⁷⁵ Tuliychukua makanisa yetu na kuunda madhehebu, nasi ni wafuasi wake, na kutulia mumo humo kama hao wengine. Na sasa, tulizoea kusema, “Mbaptisti wa kale, baridi, wa kawaida,” na sasa Wabaptisti wanasema, “Enyi Wapentekoste baridi, wa kawaida.” Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa, Pentekoste ni ya kawaida kuliko Wabaptisti. Naam, bwana. Kwa hiyo sisi hapo.

¹⁷⁶ Tunachotaka ni uamsho mzuri, wa mtindo wa kale, unaotikisa kote nchini, kuwarudisha wanaume na wanawake kwa Mungu. Mbona, Kanisa lilikuwa katika hali nzuri zaidi kwa kuja kwa Yesu miaka arobaini iliyopita, kuliko ilivyo leo, huko nyuma wakati walipokuwa na Pentekoste halisi

miongoni mwa watu. Lakini leo hii tumedhoofisha njia yetu, na mimbara zetu zimekuwa dhaifu, na makundi manne au matano ya maskini wahudumu wa seminari wameingia wakiwa na nywele pindokombo, mwajua, ama kadhalika, bila kusema lolote juu ya hilo kwa sababu sina lolote, bali hilo halileti, si... Lakini ninalomaanisha kusema, wanafikisha hilo mahali, kana tu kwamba Mungu alikuwa na wajukuu, Mungu hana wajukuu.

¹⁷⁷ Mnajua, Wamethodisti, kama wewe ni Mmethodisti na umezaliwa mara ya pili, wewe ni Mwana wa Mungu. Lakini unapata nini? Wesley akaja, awamu ya kwanza ya Methodisti ilikuwa sawa, awamu ya pili wakaanza kuwaingiza watoto wao, hilo ndilo jambo lile lile Wapentekoste walilofanya. Miaka michache iliyopita, walikuwa na Pentekoste halisi, wanaume na wanawake waliofika madhabahuni na kulipa gharama, kisha wakapitia, ndugu, na kuishi hayo maisha. Naam, bwana. Vema, walifanya nini? Waliwaingiza watoto wao ndani, wakawaweka kwenye safu, na kuwaweka wakfu kanisani, nao walikuwa Wapentekoste, hao ni wajukuu.

¹⁷⁸ Hakuna mahali katika Biblia ambapo Mungu ana wajukuu. Yeye si Babu, Yeye ni Mungu, Yeye ni Baba. Haleluya! Na kila mwanamume na mwanamke, sijali wewe ni nani, ama, jinsi baba na mama yako walivyokuwa wazuri, huna budi kuwa na tukio lilo hilo la kuzaliwa mara ya pili na kujazwa na Roho Mtakatifu kama kamwe unatarajia kuwa mwana ama binti wa Mungu. Hiyo ni kweli.

¹⁷⁹ Neno *Pentekoste* tu halitakuokoa. *Pentekoste* si dhehebu, *Pentekoste* ni tukio kwa yeyote atakaye, na aje, anywe kutoka kwenye Chemchemi ya Maji ya Uzima. Amina. Sasa, hiyo ni kweli, rafiki. Hizo ni sassafrasi kama...Je, mna sassafrasi huku juu? Vema, mnajua ninalomaanisha. Nilisema jambo hilo wakati mmoja, jamaa fulani akasema, mtu mmoja akaniandikia barua, kasema, "*Sassafrasi* ni nini?" Vema. Lakini mnajua ni nini huku juu. Naam, bwana. Loo ila, ndugu, nitakwambia, ita—itawanyosha, ita—itakufanya uishi vizuri. Hiyo ni kweli. Shuka tu kule chini, na ukae mpaka itakapokwisha, ndipo upate kunyoshwa pamoja na Mungu, naam.

¹⁸⁰ Naye Simeoni, siku hizo alikuwa, alikuwa na ahadi hiyo, naye alikuwa akiiamini kwa moyo wake wote. Yesu alizaliwa Bethlehemu ya Uyahudi (Wale mamajusi walikuja, hawakuwa na magazeti.), ndipo siku nane baadaye mama akaja hekaluni kutoa hua au njiwa kwa ajili ya utakaso, tohara ya mtoto. Na sasa huyu hapa Yesu anakuja, sasa katika kufunga, huyu hapa Yesu anakuja, mara Yake ya kwanza hekaluni mikononi mwa maskini mama Yake.

¹⁸¹ Wananiambia nguo Zake za kitoto zilitengenezwa kwa, kile kitambaa kilichofungwa nyuma ya nira ya maksai iliyokuwa imetundikwa zizini, na halafu tunaweza kuvaa koti la manyoya

ya cheche la dola mia tano na kuinua pua yetu juu hewani, kama ingelizamisha ingetunyeshea, huku tunafikiri sisi ni watu fulani, naye Mwokozi wetu, Mungu wa Mbinguni, alikuja amevikwa nguo za kitoto za maksai.

¹⁸² “Mbweha wana matundu, na ndege wana viota, lakini Mwana wa Adamu hana mahali pa kulaza kichwa Chake.” Halafu tunawazia sisi ni watu fulani, tunaweza kuendesha gari zuri kuliko la akina Jones, na karibu tuwaue tu watoto wetu kwa njaa, tupate kununua gari hilo, pia, kununua televisheni bora zaidi, ama chochote kile, tunakaa nyumbani Jumatano usiku tushuhurie mkutano wa maombi, na kuacha kanisa tupu tukiangalia *Tunampenda Susie*, ama kipindi kama hicho kinachoelelea, upuuzi huu kwenye televisheni; hiyo inaonyesha kwamba unampenda Mungu kiasi gani.

¹⁸³ Nitakwambia, ndugu, ni... tunachohitaji ni uamsho, hiyo ni kweli kabisa. Huo ndio taifa hili linaohitaji, ni kumrudia Mungu. Naam, bwana. Unapo—unapojitokeza... Matendo yako yanaonyesha ni kitu gani, matendo ya watu yanaonyesha, hasa kabisa. Ukiipenda dunia, ama mambo ya ulimwengu, Biblia inasema kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako. Hiyo ni kweli. Loo, unajiunga na kanisa, hiyo ni kweli, bali *Hili* ndilo tunalonena habari Zake, hujiungi na *Hili*, unazaliwa ndani Yake. Nimekuwa katika familia ya Branham miaka hamsini na mmoja, kamwe sikuombwa, kujiunga na hiyo familia. Kwa nini? Nilizaliwa humo, ni—nilikuwa Branham kwa kuzaliwa. Hivyo ndivyo ulivyo Mkristo, umezaliwa katika Kanisa la Mungu aliye hai, unazaliwa humo kwa kuzaliwa, wewe ni Mkristo kwa kuzaliwa.

¹⁸⁴ Sasa, Yesu aliingia hekaluni, nami ninaweza kuwawazia hao akina mama katika siku hizo, mwajua, wote huko juu pamoja na watoto wao wachanga wakiwa na vijiatu vyao, na maskini mishono yao, mwajua, na yote tayari, vijiblanketi vyao vidogo vya kupendeza, na wanawake wa jamii, mwajua, wakiongea juu ya... Basi muda si muda mwajua, akaja maskini Mariamu amembeba huyu Mtoto mchanga kwa nguo hii ya kitoto, mnaona, amezungushiwa zilizotoka kwenye nira ya maksai. Akapitia hapo, ninaweza kuwasikia baadhi yao wakisema, “*Hei! Psst! Psst!* Angalieni pale, mnamwona yule mtakatifu anayejifingirisha?” Ama, mnajua kile mimi... Labda hilo ni kosa, pia.

¹⁸⁵ Lakini ninasema, kasema, “Mwangalie mwanamke yule. Mnajua nini? Aliolewa... Huyo mtoto alizaliwa nje ya ndoa takatifu. *Hmm!* Usiniambie! Palipo na moshi kidogo, hapana budi pawe na moto mahali fulani. Naam, bwana. Nitawaambia, jamani, ni hayo tu. Naam, nawaambia, yeye ni mmoja *wao*, heri mumwangalie, mnaona. Msimkaribie.”

¹⁸⁶ Hivyo ndivyo mwaminio vuguvugu anavyojaribu kumfanyia

mwaminio halisi, “Loo, ana kichaa, amerukwa na akili, kuna kasoro. Aa, anamtumainia Mungu kwa ajili ya jambo *hili*, alisema. Aa, siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu.” Hmm! Vema.

¹⁸⁷ Lakini katika maskini moyo wake yeye alijua Mtoto huyo ni wa Nani, alijua. Na vivyo hivyo kila mtu aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu, anajua mahali anaposimama, anajua ni ufunuo gani, ni Nani anayempa ufunuo huo. Paulo alisema, “Sikuja kwenu kamwe, nikiwahubiria maneno ya kushawishi ya mwanadamu, ili hekima yenu. . . imani yenu ijengwe katika hekima ya wanadamu, bali nimekuja nikiwahubiria nguvu za Roho Mtakatifu.” Amina. Jambo ndilo hilo, ndugu, rahisi na dhahiri, wazi tu kuliadini, hivyo tu. Mungu alisema hivyo, na hilo latosha, hilo—hilo ndilo jambo lote.

¹⁸⁸ Alijua Mtoto huyo alikuwa ni wa Nani, haidhuru yeyote wa hao wengine. . . Ninaweza kuwaona wakisema, “Sasa, kaeni mbali, msimkaribie. Msiwe na uhusiano wowote naye, yeye, jitengeni tu naye.”

¹⁸⁹ Hakujali kama walimpokea ama la, haikumletea tofauti yoyote, alijua Mtoto huyu alikuwa ni wa Nani. Alijua Huyu alikuwa ni Nani. Hiyo ni kweli.

¹⁹⁰ Mnajua nini? Ulipompata Roho Mtakatifu, unajua kilichokupata, ulikuwa pale, unajua Yeye alitoka wapi. Hakutoka kwenye seminari fulani, wala makaburini, ame. . . ame—ametoka—ametoka kwa Mungu. Vema, pote pawili karibu ni sawa, mahali pa wafu, kwa hiyo basi, kumbukeni hilo.

¹⁹¹ Kwa hiyo basi, alijua mahali Mtoto huyu mchanga alikotoka. Akaangalia, naye akasema, “Naam, bwana.” Alijua, alienda akitembea, namna hiyo, bila kujali, akizungumza na Mtoto wake, hakuwa na wakati wa kushirikiana nao, mashirika hayo yote.

¹⁹² Hiyo ndiyo shida ya kanisa letu siku hizi, wana shirika la akina mama, shirika la wanaume, shirika *hili*, na michezo ya mpira, milo ya supu, na kila kitu kingine, na mikutano ya maambi inaachiliwa, mwajua. Hakuna tena. . . Naye Roho Mtakatifu aliahidi atawatia muhuri tu wale waliougua na kulia kwa ajili ya machukizo yaliyofanywa mjini.

¹⁹³ Enyi makasisi, ungeweza kuandika mkononi mwako watu kumi, usiku wa leo, katika mji huu wanaougua na kulia, mchana na usiku, kwa ajili ya uovu na kadhalika yanayotendeka mjini? Kuna mtu katika kusanyiko hili anayejua mahali unapoweza kuelekeza vidole vyako juu ya watu watano wanaougua na kulia, mchana na usiku, kwa ajili ya dhambi, na mambo ya huu mji? Vema sasa, Biblia ilisema uweke alama juu ya wale wanaougua na kulia kwa ajili ya machukizo yanayofanywa mjini. Hiyo ni kweli. Jambo ndilo hilo. Mnaona?

¹⁹⁴ Hakuna mzigo tena kwa ajili ya nafsi zilizopotea, wote umetoweka, tu—tulijiunga tu na kanisa na kutulia, “Hayo ndiyo yote yanayohitajika.” Mnaona? Hivyo ndivyo tunavyopata. Ni ninii sana, dhambi ni nyemelezi sana, nayo inakunyemelea kisirisiri kabla hujajua, unaona, hivyo ndivyo inavyofanya. Inakunyakua tu kama vile ile sileji telezi ya kale ilivyokuwa, nayo imekushika, ibilisi hufanya hivyo.

¹⁹⁵ Sasa, ndugu, hebu turudi moja kwa moja kutoka kwenye eneo lake, hebu tumrudie Mungu, turudi madhabahuni, tujenge upya madhabahu tena ambayo imebomolewa. Ijenge nyumba yako, ondoa hizo karata mezani, na hayo magazeti yote ya hadithi za mapenzi, kisha uifungue Biblia, na kuisoma Biblia, na—na—na kuomba, kamwe usishuke tu chini na kusema, “Ibariki familia yangu, na Mary, na Joe, na John, na hao wote,” uruke kitandani, la, bwana, kaa hapo pamoja na Mungu. Loo, jamani!

¹⁹⁶ Unajua ule wimbo uliozoea kuimba, “Kuna nyakati ningependa kuwa peke yangu pamoja na Kristo Bwana wangu, naweza kumwambia Yeye shida zangu zote peke yangu kabisa”? Hilo ndilo tunalohitaji tena, hilo ndilo, mikutano ya namna hiyo, kanisa la namna hiyo, hiyo ndiyo aina ya kanisa ambalo huomba baraka za Mungu zikashuka. Nina hakika mchungaji wenu angefurahia kila mshiriki akiwa hivyo. Jinsi ambavyo angeninii...! Na jinsi ingekuwa kama kanisa lingeweza tu kuwa hivyo tena!

¹⁹⁷ Sasa anakuja pamoja na Mtoto huyu mchanga, sasa huyo hapo Kristo hekaluni. Vema, kama Kristo yuko hekaluni, na Mungu alikuwa amemfunulia Simeoni kwamba yuko, Yeye atamwonyesha Kristo kabla hajafa, vema, nafikiri kama Kristo yuko hekaluni, wakati umewadia kwa Roho Mtakatifu kuanza kumshughulikia Simeoni. Hivi hamwoni hivyo?

¹⁹⁸ Hebu tuwazie ni Jumatatu asubuhi. Sasa, ni watoto wangapi wachanga wangezaliwa? Kuna yapata watu milioni mbili na nusu katika Israeli wakati huo, nami nadhani kungekuwako na angalau mamia ya watoto wachanga wanaozaliwa kila usiku, na kila siku nane iliwabidi kutahiriwa, na kutolewa sadaka ya utakaso. Vema.

¹⁹⁹ Hawa hapa sasa, ni Jumatatu asubuhi, Simeoni amerudi ofisini, akisoma Magombo. Hebu tuone, anachukua Isaya, naye anaanza kusoma hadi Isaya 9:6, “Kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa Mwana, ataitwa Jina Lake Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele, uweza wa kifalme utakuwa mabegani Mwake. Na ninii...’ Loo, huyo angeweza kuwa ni Nani?”

Yapata wakati huo Roho Mtakatifu akasema, “Simama, Simeoni.”

“Ati nisimame? Unataka nifanye nini?”

“Simama tu.”

“Vema, niende wapi?”

²⁰⁰ “La, wewe simama tu, hayo ndiyo tu ninayotaka ufanye.” Hivyo ndivyo Mungu anavyokutaka, jinsi tu asemavyo, nenda ukatekeleze. Hivyo ndivyo unavyotaka kufanya juma hili, Mungu anaponena, tekeleza, lifanye. Aseme, “Nenda ukamwone *Fulani-wa-fulani* kuhusu kuja kanisani.” Tekeleza, fanya hivyo.

“Simama.”

“Naam, Bwana, mimi hapa.”

“Nini tena?”

“Anza kutembea.”

“Wapi?”

“Tembea. Mimi nitaongoza, wewe tembea.” Unaona?

²⁰¹ Huyu hapa anakuja, namwona akitokea akishangaa, “Vema, ninajua huyu ni Roho Mtakatifu, maana Yeye amenena nami hapo awali.” Mnajua ninalomaanisha, sivyo? Mnaamini wana wa Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu? Naam, wanaongozwa. Huyu hapa anakuja akitembea, akitembea kupitia hekaluni, bila kujua anakoelekea, akiongozwa tu na Roho Mtakatifu. Sasa, yeye anakuja, na kushuka kupitia maelfu ya watu kila mahali, hapa anafikia mstari huu wa tohara ya watoto, akija, akitembea moja kwa moja kwenye mstari huu.

²⁰² Anamwona maskini mwanamke huyu ambaye kila mtu anajitenga naye, yeye anapanda. Roho Mtakatifu anaanza kuufanya moyo wake upige upesi sana, mwajua. Loo, Yeye anakuongoza kwenye ile ahadi. Naam. Kama alikupa ahadi, nawe unaamini katika uponyaji wa Kiungu, Yeye anakuongoza moja kwa moja ndani yake. Kama unaamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, Yeye anakuongoza moja kwa moja ndani yake. Unaona? Mahali ulipo, Yeye atakuongoza moja kwa moja kwake.

²⁰³ Sasa, Yeye amemfikisha papa hapa, karibu naye. Simeoni ananyosha mkono, anamchukua Mtoto huyo kutoka mikononi mwa mama Yake, anainua mikono yake, na kusema, “Mungu, jalia mtumishi Wako aondoke kwa amani, kulingana na Neno Lako, kwa kuwa macho yangu yameuona Wokovu Wako.”

²⁰⁴ Huko nyuma kabisa, huko pembeni, mwanamke mkongwe, kipofu, jina lake Ana, yeye alikuwa ni nabii mke, Ana alikuwa nabii mke, alikuwa kipofu kwa miaka mingi, aliketi pale, naye pia alingojea na kuamini faraja ya Israeli, aliamini ya kwamba Nabii huyo alikuwa yuaja, naye alikuwa anaamini. Alikuwa ameketi pale, ndipo Roho Mtakatifu akasema, “Ana, simama.” Amina. Wale walio wa kiroho daima wanaongozwa, mwajua, kwa wakati unaofaa. “Simama, Ana.”

Naye huyu hapa anakuja maskini mwanamke huyu mkongwe, kipofu, “Samahani, bwana. Samahani, mama. Kunradhi.” Akiongozwa na Mtakatifu...

“Unaenda wapi, Ana?”

“Sijui, ninaongozwa tu.”

²⁰⁵ Muda si muda mwajua, anakuja moja kwa moja hadi mahali Simeoni amesimama, na kusema, “Bwana, mruhusu mtumishi Wako aondoke kwa amani.” Yeye, vivyo hivyo, Roho Mtakatifu alimshukia, naye akaanza kutabiri juu ya yule Mtoto.

²⁰⁶ Loo, ndugu, dada, kama Roho Mtakatifu angeweza kumwongoza mwanamke kipofu katika nyakati kama hizo, ni kiasi gani anapaswa kutuongoza? Ingawa tunakuwa vipofu, na atuongoze kuturudisha kwenye ile Chemchemi.

Kwa kuwa kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
Ambapo wenye dhambi wakitumbukia chini
ya hiyo gharika,
Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

²⁰⁷ Mnaamini hilo? Mungu awabariki. Je, mnatarajia jambo fulani kutukia? Muda wangu umekwisha. Sasa, ninyi ni kusanyiko zuri sana, ningeweza kuzungumza nanyi saa moja bado, lakini muda wangu umekwisha. Na hebu tuwe tukimtarajia Mungu kutupa uamsho mkuu. Je, mta—mtaungana nami katika maombi, kwa kusudi hilo? Mtafanya hivyo? Na tuinamishe vichwa vyetu basi.

²⁰⁸ Sasa, ndugu wahudumu, najua ninyi nyote mnautarajia. Tuko hapa kufanya kazi pamoja kama umoja wa Mungu, tusiache chochote kisimame njiani mwetu sasa.

²⁰⁹ Enyi Kanisa, tuko hapa kufanya kazi pamoja nanyi, ninyi nyote mlilo wa Assemblies of God, na Church of God, na United Pentecostals, na chochote uwezacho kuwa, hatujali unavaa chapa gani, tuna—tunaamini tu kwamba Mungu atafanya hivyo. Hebu na tuungane pamoja sasa katika moyo mmoja.

²¹⁰ Baba yetu wa Mbinguni, maneno haya yaliyovunjika-vunjika na mazungumzo kidogo hapa, kusudi tu kwa namna fulani kuondoa woga wote na ugumu kutoka kwa Kanisa Lako, kwa namna fulani kuchimba tu shamba lililolimwa ili kuweka msingi hapa, ama si kuweka msingi, bali kujenga juu ya Msingi ambao tayari umewekwa, Kristo Yesu, yale watu hawa wamefundishwa kuamini kote katika miaka, ya kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

²¹¹ Baba wa Mbinguni, ninaomba, tunapounganisha mioyo yetu na maombi yetu pamoja, Biblia ilisema katika mlango wa nne wa, ninaamini, wa Matendo ya Mitume, watu walipokuwa wamekusanyika, walitoa taarifa, kisha wakaomba kwa

moyo mmoja, nalo jengo likatikisika mahali walipokuwa wamekusanyika pamoja, nao wakanena Neno la Mungu kwa ujasiri.

²¹² Ee Mungu, tunaendelea hapa, leo, tukiwa tumebandikwa jina hili zuri sana, kama waaminio wa Kipentekoste, tukishuhudia ya kwamba tumezaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu, naye Roho Mtakatifu anatuongoza. Ndipo, Bwana, kuona kanisa likidhoofika, na kuanguka, na kuporomoka, na, Ee Mungu, ni—ni hali ya jinsi gani! Tuhuishe, Ee Bwana, mtume Roho Wako Mtakatifu juu yetu, na ulete kuburudishwa, matone ya umande wa rehema kutoka juu.

²¹³ Ee Mungu, ihuishe jamii ye—ye—yetu hapa, uhuishie mji mzima, yahuishe makanisa huku kote, wahuishie Wamethodisti, wahuishie Wabaptisti, wahuishie hao wote, Bwana. Na, Ee Mungu, jalia uanzie papa hapa katika kusanyiko hili, jalia kuwe na uhuisho na uamsho mkubwa sana miongoni mwetu, Bwana, mpaka Roho Mtakatifu aichukue mioyo yetu, na kutuvunjilia mbali, na kumimina kutoka kwetu marhamu ya thamani ambayo Yeye angetaka Kanisa letu lipakwe. Tujalie, Bwana.

²¹⁴ Tubariki sasa. Tusamehe dhambi zetu, kupungukiwa kwetu. Mungu, jalia kusiwe na mgonjwa atakayehudhuria mkutano huu, ila ambaye ataponywa. Tujalie, Bwana. Jalia kamwe kusiwe na mtu mmoja ambaye ni mwenye dhambi, ama asiyeamini atakayehudhuria mkutano huu, ila ambaye ataokolewa. Tujalie, Bwana.

²¹⁵ Malaika wa Mungu na waende kwenye kila kanisa kote katika hii jamii, kila mahali, washuke kwenye vyumba vya pombe, na—na kuleta hukumu juu ya wenye dhambi. Pia jalia Wakristo waende wakashuhudia, wakisema, “Njoni, mwone! Njoni, mwone! Hatujawahi kuona kitu kama hicho.” Tujalie, Bwana. Jalia uwe ni mngurumo mkuu kote katika nchi hii, na Mungu akipata utukufu kutoka kwake. Tujalie, Baba.

²¹⁶ Wabariki wachungaji Wako wa thamani, naomba tena, hapa nyuma, nikisimama hapa jukwaani, wengine sijawahi kuwaona maishani mwangu, lakini, Bwana Mungu, wanasimama hapa kutoa ushuhuda ya kwamba wao, pia, ni waaminio, wako hapa pamoja na, wapate kuchangia sehemu yao, kusaidia mwendeleo. Mioyo yetu inawaka na kutamani, Bwana, tunamwona Roho wa Mungu akitenda kazi miongoni mwetu. Tujalie. Fanya haya kwa ajili yetu, Baba. Tunajikabidhi Kwako, katika Jina la Kristo. Kwa ajili ya utukufu Wake tunaomba hayo.

²¹⁷ Sasa wote walio humu ndani walio wagonjwa na wahitaji, inueni mikono yenu, sasa hivi, inueni tu mikono yenu. Vema. Ninawatakeni mwekeane mikono, wekeaneni tu mikono sasa. Baadhi... Sasa, usijiombee, wewe mwombee mtu uliyemwekea mkono wako, wanakuombea. (Ninapenda hilo, “Mambo yote yanawezekana.”)

218 Sasa, ndani—ndani ya mioyo yetu, hebu tuwazie tu sasa. Ninaweza kuona ku—kundi la wanafunzi wamemzunguka m—mvulana mwenye kifafa. Ninaweza kumsikia Andrea akisema, “Rudini nyuma, enyi wavulana, ni—nitawaonyesha jinsi nilivyofanya huko Kapernaumu, nilipofukuza kifafa kule chini. Hivi ndivyo nilivyofanya!” Lakini haikufanikiwa.

219 Simoni Petro akajongea, kasema—kasema, “Vema, sasa, hivi ndivyo nilivyofanya huko chini Yafa, nitawaonyesha jinsi nilivyofanya huko chini.” Wala haikufanikiwa.

220 Lakini ilitokea walimwona akishuka kuja chini ya kilima, Mmoja akitembea, kwa utulivu, labda hakuonekana Mtu mkubwa, kama jitu, lilisema, “Hana uzuri, hata tumtamani.” Lakini kuna jambo fulani kumhusu Yeye, alijua alichokuwa anazungumzia. Ndipo akamkimbilia, huyu baba wa huyo mtoto, na kusema, “Bwana, umrehemu mwanangu, amepagawa sana na pepo. Nilimleta kwa wanafunzi Wako, wasingeweza kumponya.”

Yesu akasema, “Ninaweza, kama ukiamini, kwa kuwa mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio.”

Kasema, “Bwana, naamini; saidia kutokuamini kwangu.”

221 Mtu yuyo huyo, wakati alipouacha ulimwengu, Mwokozi wetu, yale Maneno ya mwisho aliyosema, “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Ishara ya mwisho aliyosema, Yeye alisema, “Wataweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.”

222 Sasa, kuna mwaminio aliyeweka mikono yake juu yako, mwaminio anayeamini katika uponyaji. Yesu alitoa tamshi hili: “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Sasa kama unaamini kwa moyo wako wote, usiwe na shaka, ninii, na uombe maombi ya imani, basi yule ambaye, ambaye umemwekea mikono yako anakuombea, naamini.

223 Baba yetu wa Mbinguni, tunaweka mikono yetu, kwa imani, juu ya wagonjwa na wanaoteseka, na kuomba kwamba neema Yako na rehema zitawapa kila kitu wanachohitaji. Wanaomba, Bwana, jinsi tu wanavyofanya kanisani mwao; wanakupenda, na wanakuamini. Ninaomba, Baba wa Mbinguni, kwa moyo wangu wote, ya kwamba utavunja kila pingu ya kutokuamini, umtoe kila pepo mchafu, jalia wasiweze kusimama ndani ya hili jengo, Bwana, mwondoshe. Jalia pasiwepo na chochote ndani ya kila moyo, ila imani safi, isiyoghoshiwa katika Mungu, sasa hivi. Ibilisi na ashindwe maishani mwetu, nasi tunajua ameshindwa, kwa sababu yeye ndiye kiumbe kilichoshindwa.

224 Na, Shetani, ninakugeukia sasa kusema hivi, ya kwamba umeshindwa, hutuogopi sisi, bali unamwogopa Yule tunayenena habari zake. Umepoteza kila nguvu uliyowahi kuwa nayo, ulishindwa pale Kalvari, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alishinda kila adui, alishinda magonjwa yote, mauti yote,

kuzimu, na kaburi, na kushinda kila ushindi uliowahi kupata. Nawe si kitu ila laghai, nasi tunasai udanyanyifu wako, usiku wa leo. Katika Jina la Yesu Kristo, waachilie watu hawa, wana—wanafuata kabisa na wanatarajia kuponywa, nguvu za Mungu zipo, waaminio wamewekeana mikono. Shetani, waache hao watu, toka ndani yao, katika Jina la Yesu Kristo, umeshindwa vita.

225 Nao watakuwa wazima kwa sababu Mungu alisema hivyo, Mungu aliahidi hilo, tunalitarajia, nasi tunajua itakuwa hivyo, maana Shetani ameshindwa, naye Mungu ana mamlaka. Tunajua ya kwamba ndivyo ilivyo, kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu Kristo, iwe hivyo, kwa utukufu wa Mungu.

226 Sasa kaa tu umefungiwa ndani na Mungu, endelea tu kuamini sasa, kwa moyo wako wote, “Bwana, ninaamini ya kwamba Wewe umeniponya sasa hivi. Ninaamini, kwa sababu nilimwekea mwanamume huyu *hapa* mkono wangu, aliniwekea mkono wake, ama juu ya mwanamke huyu, aliniwekea mkono wake, niliongozwa kufanya hivyo, niliongozwa kuwekea mtu huyu mkono wangu, waliongozwa kuniwekea mikono yao, Roho Mtakatifu yeye yule aliyemwambia Simeoni, akampa ile ahadi, aliniongoza kufanya hivi wakati tukiwa papa hapa katika mahali hapa pa uponyaji wa Kiungu. Sasa ninaamini, Bwana.

227 “Shetani, afadhali uniondokee sasa hivi, kwa sababu ninachukua... Mimi ni Uzao wa Ibrahimu kwa njia ya Yesu Kristo, nami ninachukua nafasi ya kwanza.”

228 Endelea tu kuamini kwa moyo wako wote, huku nikimwomba mmoja wa wachungaji wetu hapa, yule, yule, mmoja wa ndugu hawa hapa, tafadhali, kama utakuja kuomba dua. Baadhi, mmoja wa wachungaji hapa, aje achukue ibada, mmoja wenu hapa. Vema, bwana.

229 Mpaka... Wasikilizaji, jifungieni ndani na Mungu kwa dakika chache tu. Ninataka kuwaulizeni sasa, mnapoondoleana mikono yenu, na kusema, “Nimeamini, na ninamchukua Yeye, sasa hivi, kama Mponyaji wangu, na haidhuru Shetani atajaribu kuniambia nini, nitaamini ya kwamba Mungu ananiponya,” inua mkono wako, useme, “Sasa ninaukubali.” Inua mkono wako. Mungu awabariki. Hiyo ndiyo njia ya kulifanya. Dumisheni imani ya namna hiyo ikiendelea, nanyi mtaona mambo mengi sana, kwa wingi, zaidi ya yote ambayo hata tungeweza kufanya ama kuwazia. Mpaka nitakapowaona kesho usiku, huyu hapa mchungaji. Mungu awabariki. 

61-0308 Matarajio
Lyric Building
Richmond, Virginia Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org